epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumatano Aprili 17, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581649
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



**MAN CITY KAMILI KUIVAA MADRID LEO**

UKURASA 22

# Mikopo halmashauri sasa kuja kivingine

• **Kuanza** majaribio mamlaka 10, kamati hadi vijijini... *Endelea ukurasa 2*

UKURASA WA 22



**POCHETTINO AKERWA NA UTOTO WA WACHEZAJI**

USHINDI wa mabao 6-0 ikiwa ni pamoja na usiku wa mabao manne kwa mmoja wachezaji wake nyota, Cole Palmer -ungemwacha Kocha wa Chelsea, Mauricio...

**Uhaba** mkubwa mafuta petroli watikisa Zanzibar



UKURASA 2

**Ripoti** CAG yabaini ulaji wa mabilioni



UKURASA 3

**Kioja** mwalimu akitimua mbio kukwepa wadai waliofika shuleni

UKURASA 7

## Manung'uniko ya malipo, lawama ubomoaji nyumba bonde la Msimbazi

UKURASA 3



Mkazi wa eneo la Jangwani, Kata ya Mchikichini, Zahor Mohamed (mwenye kanzu nyeusi), akisimamia ubomoaji wa nyumba yake, ili kupisha Mradi wa Bonde la Msimbazi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: ROMANA MALLYA**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akiwa kwenye helkopta wakati akikagua athari zilizosababishwa na mafuriko yaliyotokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha nchini katika maeneo ya Taweta, Masagati, Utengule na Malinyi, Halmashauri ya Mlimba, Wilaya ya Kilombero mkoani Morogoro jana. **PICHA: OWM**



## Serikali yasikia kilio cha wafanyakazi kikokotoo

UKURASA 2

**MICHEZO** **BENCHIKHA ACHAMBUA WASHAMBULIAJI** UK.24

**KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Mikopo asilimia 10 kurejea kivingine

**Na Vitus Audax,** DODOMA

MIKOPO ya asilimia 10 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu inatarajiwa kuanza kutolewa tena kuanzia Julai, mwaka huu, kwa utaratibu mpya wa kutumia benki kwa halmashauri 10 za majaribio.

Waziri wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mohamed Mchengerwa, alisema jana bungeni jijini hapa, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2024/25.

"Ninapenda kumshukuru Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa kurejesha utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuanzia Julai, 2024 kwa utaratibu wa kutumia benki kwa halmashauri 10 za majaribio," alisema.

Mchengerwa alitaja halmashauri hizo kuwa ni majiji ya Dar es Salaam na Dodoma, Manispaa za Kigoma/Ujiji na Songea, miji ya Newala na Mbulu, wilaya za Siha, Nkasi, Itilima na Bumbuli.

Mchengerwa alisema halmashauri 174 zilizobaki zitatumia utaratibu ulioboreshwa, ili kuondoa upungufu uliosababisha changamoto za awali.

Alisema maboresho yanatarajiwa kufanyika ikiwamo uanzishwaji wa kitengo cha usimamizi wa mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu katika OR-TAMISEMI na uanzishwaji wa kamati za usimamizi wa mikopo katika ngazi za ofisi za wakuu wa mikoa, halmashauri na kata.

Pia alitaja majukumu ya kamati ngazi ya kata kuwa itakuwa ni pamoja na kutambua waombaji na kuthibitisha vikundi vya mikopo na kuvisajili kwenye mfumo kabla ya kuwasilisha kwenye kamati ya halmashauri.

Alisema kazi zingine zilizofanyika ni pamoja na kusanifu na kujenga mfumo mpya unaoitwa 'Wezesha Portal' utakaotumika kwa ajili ya taratibu za ukopeshwaji wa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Alisema mfumo huo utaondoa changamoto za mfumo zilizokuwapo awali kabla ya mikopo kusimamishwa.

"Maboresho mengine yaliyopangwa kufanyika ni kujenga uwezo kwa wasimamizi wa mikopo hiyo kwa kuongeza idadi ya wasimamizi wa mikopo kwenye ngazi ya kata ambapo maofisa maendeleo ya jamii 787 wameajiriwa na kupangiwa kata zilizokuwa na upungufu," alisema.

Alisema watumishi hao na timu nzima itakayosimamia mikopo hiyo katika ngazi zote itapatiwa mafunzo na wataalamu wabobezi wa usimamizi wa mikopo ya aina hiyo.

Kadhalika, alisema ofisi hiyo imepanga kurekebisha sheria inayosimamia mikopo hiyo na kanuni zake ili kuongeza ufanisi. Baada ya kipindi cha mpito, tathmini itafanyika ili kubaini mfumo bora utakaotumika katika utoaji wa mikopo hiyo.


Alisema mikopo inayotarajiwa kutolewa ni Sh. bilioni 227.96 kati ya hizo, Sh. bilioni 63.67 ni fedha za marejesho zilizokuwa zikiendelea kukusanywa kutokana na mikopo iliyotolewa kabla ya kusimamishwa.

Sh. bilioni 63.24, alisema ni fedha zilizokuwa zinatengwa kwa ajili ya mikopo na Sh.bilioni 101.05 ni fedha ambazo zimetengwa kutokana na makisio ya makusanyo ya mapato ya ndani ya mwaka 2024/25.

"Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kuzisimamia mamlaka za serikali za mitaa kukusanya marejesho kutoka katika vikundi vilivyokopeshwa fedha za asilimia 10 na Sh. bilioni 43.77 zitakusanywa kutoka katika vikundi vinavyoendelea kufanya marejesho," alisema.

Pia alisema mikopo hiyo itasimamiwa kwa umakini kuhakikisha hakuna vikundi hewa na yeyote atakayepatikana na ubadhirifu wa aina yoyote atachukuliwa hatua za kisheria.

"Kama waungwana wasemavyo" 'Akopaye akilipa huondokana na lawama.' hivyo ninapenda kuwaelekeza wakuu wa mikoa kusimamia kwa makini mikopo hiyo,"alisisitiza.



Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda akimvalisha koti Askofu Mkuu mstaafu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Kardinali Polycarp Pengo, alipomtembelea ofisini kwake jijini Arusha juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yasikia kilio cha kikokotoo

**Na Vitus Audax,** DODOMA

KUTOKANA na kuibuka upya kwa mijadala mbalimbali ndani na nje ya Bunge kuhusu kanuni mpya ya kikokotoo kipya cha mafao ya wastaafu, serikali imesema imepokea maoni yote yaliyotolewa na wadau pamoja na wabunge na kuahidi kufanyia kazi.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema hayo juzi bungeni wakati wa kuhitimisha hoja ya makadirio ya Mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa mwaka 2024/25.

Majaliwa alisema hoja zilizoibuliwa na wabunge wakati wa uchangiaji wa hotuba yake ya makadirio ya mapato na matumizi, ikiwamo ya ulipaji wa mafao ya wafanyakazi kupitia mifuko ya hifadhi ya jamii, serikali imesikia na kupokea maoni mbalimbali ya wadau wakiwamo wabunge, wafanyakazi na vyama vya waajiri na wafanyakazi.

Alisema serikali inatambua umuhimu wa kuboresha mafao kwa wastaafu na itaendelea kufanya tathimini kwa kuzingatia sheria za kazi.

Pia alisema serikali itaendelea kutoa elimu ya hifadhi ya jamii ikiwamo mafao kwa watumishi kupitia njia mbalimbali na waziri wa kazi na ajira kusimamia na kuongeza wigo wa utoaji wa elimu ya mafao kwa watumishi kwa lengo la kujenga uelewa wa kutosha kuhusu.

Kuhusu hoja ya serikali kupunguza uhaba wa walimu ili kuendana na mitaala mipya ya elimu, iliyojibiwa na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, alisema serikali imeendelea kuboresha mazingira ya walimu pamoja na kutoa fursa mpya za ajira.

Alisema kwa mwaka 2023/24 serikali ilitoa nafasi za ajira 10,505 za walimu na kwa mwaka 2024/25 inatarajia kufoa ajira mpya kwa walimu 10,590, ili kutatua kwa kiwango kikubwa kero zilizoko katika eneo hilo.

Akizungumzia hoja ya serikali kuweka mikakati ya upatikanaji wa vyanzo vingi vya mapato ili kuwezesha bima za afya kwa wananchi wa vijijini, Waziri Mkuu alisema serikali inapokea mapendekezo yote na kuahidi kufanyiwa kazi.

Alisema Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2023 imeanzisha mfuko kwa ajili ya kugharimia bima ya afya kwa watu wasio na uwezo na kubainisha vyanzo vya fedha vya mfuko huo na serikali itaendelea kupokea mapendekezo ya uendeshaji wa mfuko ikiwemo vyanzo vya mapato na kufanya maboresho kadri inavyofaa.

Kuhusu wanyamapori kuvamia maeneo ya wananchi mauaji ya watu kwenye hifadhi, Majaliwa alisema serikali inatambua madhara ambayo yamekuwa yakisababishwa na wanyamapori kuvamia makazi na mashamba na madhara kwa wananchi waishio karibu na hifadhi yakiwamo ulemavu, vifo na uharibifu wa mali.

## Uhaba petroli waitikisa Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

UHABA wa petroli visiwani Zanzibar umesababisha usumbufu kwa baadhi ya wananchi wakiwamo watumiaji wa vyombo vya moto.

Uhaba huo umesababisha vituo vya kuuzia mafuta kufungwa na baadhi ya magari kushindwa kuendelea na safari baada ya kuishiwa na mafuta.

"Tangu jana gari langu limeniishia mafuta nimeiacha hapo hapo katika kituo cha mafuta," alisema Mussa Khamis, mkazi wa mjini hapa wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema kama hali hiyo itaendelea ni hatari na shughuli nyingi za kimaendeleo na kiuchumi zitasita.

Alisema pia kuadimika kwa mafuta biashara ya magendo itajitokeza na serikali kukosa mapato.

Mfanyakazi mmoja katika kituo cha kuuzia mafuta kiliopo Kisauni ambaye hakutaka kutajwa jina lake alisema kuwa uhaba wa mafuta umetokana na kuchelewa kufika kwa meli ya mafuta kutoka Tanzania Bara.

Alisema ni siku ya pili kituoni hapo hawana mafuta ya petroli na wateja wao wanafika na kuondoka.

"Tunaziomba mamlaka husika kurahakisha upatikanaji wa mafuta ili kuondokana na changamoto hii na isijitokeze tena," alisema.

Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishatii Zanzibar (ZURA), imesema kuwa upungufu wa mafuta ubesabishwa na kuchelewa kufika kwa meli ya mafuta Zanzibar kutoka Tanga ilikokwenda kupakia.

## ‘CCM haitashika dola kwa mabavu wala kwa bunduki’

**Na Halfani Chusi,** SONGWE

KATIBU Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) – Oganaizesheni, Issa Haji Gavu, amesema kamwe chama hicho hakitashika dola kwa mabavu wala kutumia bunduki bali kidemokrasia.

Gavu aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwenye mkutano uliokutanisha viongozi wa chama, serikali, taasisi ziziso za kiserikali, viongozi wa dini, wazee na machifu katika Kata ya Mlowo, Mbozi mkoani Songwe ukiwa mwendelezo wa ziara za chama hicho

“Hatutashika dola kwa mabavu wala bunduki bali tutashika dola kwa njia za kidemokrasia. Msingi wa demokrasia ni kupiga kura na ili mwanadamu ashawishike basi una wajibu wa kumshawishi kabla ya kupiga kura”, alisema.

“Tuhakikishe tunaendelea kuhamasisha na kuchapa kazi kwa kuwa ndicho kitu pekee kitakachoendelea kutupa thamani kwa wananchi kuendelea kutuamini,” aliongeza.

Wakati huo huo, katika mkutano wa hadhara mkoani hapa, Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, alisema ‘atamkaba shingo’ Waziri wa Maji, Jumaa Aweso kuhakikisha mradi wa maji mkoani Songwe unakamilika kwa wakati hyuku akisistiza kuwa lengo la Rais Samia Suluhu Hassan ni kuwatua kinamama ndoo kichwani.

Pia aliwataka watumishi wa halmashauri kutatua migogoro ya ardhi na kutenda haki, huku akimwagiza Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, kutoa kibali kwa wakulima na wafanyabiashara ili kuuza mazao nje ya nchi.

“Tuendelee kufanya kazi kwa juhudi. Ninatoa aelekezo kwa serikali inapaswa isimamie haki za raia watumishi wa halmashauri kuhakikisha wanatatua migogoro ya ardhi wasiruhusu wananchi wadhurumiwe ninawaomba sana sana.

“Habari ya maji Rais ametoa Sh. bilioni 100 ninaomba zisimamiwe vizuri nitambana Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, kuhakikisha zinafika

# Manung’uniko ya malipo, lawama ubomoaji nyumba Bonde Msimbazi

**Na Mwandishi Wetu**

BOMOA bomoa nyumba kupisha Mradi wa Bonde la Msimbazi jijini Dar es Salaam inaendelea, huku baadhi ya wakazi wakilalamikia fidia ndogo na wapangaji wakirusha lawama kwa wenye nyumba kuchukua fedha za pango, huku wakiwa wameshachukua malipo ya kuondoka.

Wapangaji wamelalamikia wenye nyumba kuchukua kodi za nyumba wakati wakiwa wametia saini serikalini malipo ya kuondoka maeneo hayo. Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi jana wakati wananchi wakiendelea na ubomoaji wa nyumba zao baada ya fidia, walisema malipo yalivyofanyika yamekuwa na sintofahamu kwao.

“Binafsi sijakataa kuondoka. Nimesaini fedha, lakini kiuhalisia fedha niliyosaini haina thamani ya ardhi yangu na nyumba yangu ninayovunja yenye vyumba vitano,” alisema Thobias Hiporiti, mkazi wa Kata ya Mzimuni, Mtaa wa Mwinyimkuu, Kinondoni, mkoani Dar es Salaam.

Hiporiti alidai awali wakati wanaelezwa kuhusu kuwapo kwa mradi huo, waliambiwa watakaopisha watapewa fedha si chini ya Sh. milioni 70, lakini ameshangaa wakati akitia saini fidia yake ameambulia Sh. milioni 34 wakati ana hati ya eneo hilo.

“Mimi nipo tofauti na wenzangu. Nina hati ya ardhi na nimekuwa nikiilipia kila mwaka. Machi 14, 2023, nilipata fidia ya awamu ya kwanza Sh. milioni 26.5.

“Novemba 2, 2023, nikapata nyongeza ya zaidi ya Sh. 800,000 na hii ni baada ya baadhi ya wananchi kugomea malipo yao kuwa ni madogo. Baadaye tena nikapewa Sh. milioni nne ambazo niliambiwa Rais ameongeza fedha hii.

“Kwa ujumla tunaondoka hapa kinyonge. Baada ya kusaini malipo nilipewa muda wa kuondoka hapa hadi Aprili 12, 2024, muda umeisha ndiyo naendelea kubomoa nyumba yangu kidogo kidogo angalau niondoke na baadhi ya vitu ambavyo vitanisaidia huko mbele badala ya kusubiri kubomolewa,” alisema.

Kibagu Juma, mkazi wa eneo hilo, alisema nyumba yao ina vyumba vitano, licha ya kupewa malipo bado hajaanza kubomoa.

“Nilishasaini fidia tangu Aprili 8, mwaka huu, ninasubiri ingie katika akaunti yangu ndipo nianze kubomoa kidogo kidogo nyumba.

“Kwa ujumla fedha niliyopewa ni kidogo nimefidiwa Sh. milioni 20, nyumba hii ilikuwa ya wazazi wetu ambao walishafariki dunia, watoto tumebaki wawili.

“Hapa kuna kugawana tena Sh. milioni 10 kila mmoja. Sasa Sh. milioni 10 unaifanyia nini kwa maisha ya sasa. Kwanza maeneo tu ya hapa tangu mchakato huu utangazwe vyumba vimepanda bei, na bei ya viwanja huko mnaijua,” alisema.

Imani Mwangunga, mkazi wa Kata ya Mchikichini, alisema nyumba yake ambayo alianza juzi kuibomoa ina vyumba vinane na vyoo viwili vya ndani na ipo ndani ya uzio.

“Nimefidiwa Sh. milioni 51 ambapo Sh. milioni 47 ni fidia ya nyumba na Sh. milioni nne fidia ya ardhi. Nikitazama nyumba hii na nilichofidiwa nikiangalia na gharama za maisha kwa sasa vitu vimepanda bei, ninaona bado sikustahili fedha ilipaswa iwe zaidi,” alisema.

Mwangunga alisema katika malipo hayo pia, amefidiwa migomba iliyoko katika ua wake Sh. 175,000, lakini choo cha nje pamoja na uzio hajafidiwa chochote.

Alisema ameanza kubomoa nyumba hiyo kwa kuwa amepewa wiki sita za kuondoka hapo tangu asaini fidia hiyo.



Rais mstaafu Dk. Jakaya Mrisho Kikwete akikaribishwa na Rais wa Uganda, Yoweri Kaguta Museveni alipomtembelea katika Ikulu ya Entebbe, baada ya kuhutubia mkutano wa chama cha viongozi wa zamani na wa sasa wa Serikali za Vyuo vya Elimu ya juu nchini Uganda, ulioandaliwa katika Chuo Kikuu cha Makerere jijini Kampala juzi. **PICHA: OFISI YA RAIS MSTAAFU**

# Ulaji mabilioni wabainika mashirika ya umma

**Na Vitus Audax,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini mashirika ya umma 17 yenye matumizi ya jumla ya Sh. bilioni 72.36 yasiyo na tija.

Kiwango hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 13 kulinganishwa na mwaka uliopita ambapo kulikuwa na mashirika ya umma 12 yaliyotumia Sh. bilioni 63.77.

CAG Charles Kichere anabainisha hayo katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2022/23 iliyowasilishwa bungeni juzi.

Anasema amebaini mashirika ya umma 11 yenye matumizi yasiyostahili ya Sh. bilioni 4.64, dosari hiyo ikiwa imepungua kwa asilimia 94 kulinganishwa na Sh. bilioni 77.75 kwa mashirika ya umma 21 mwaka uliotangulia.

Anafafanua kuwa kati ya mashirika hayo, manne yaliripotiwa pia mwaka uliotangulia. Hayo ni Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA) na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO).

CAG anasema TPA ilitumia Sh. bilioni 33.861, TANESCO Sh. bilioni 26.042, Bodi ya Pamba Tanzania (TCB) Sh. bilioni 6.563, DAWASA Sh. bilioni 3.583.

Mengine ni Shirika la Reli Tanzania Sh. bilioni 1.249, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza Sh. milioni 335.65, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) Sh. milioni 270.99, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea Sh. milioni 150.09, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida Sh. milioni 39.56,

Pia yamo Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania Sh. milioni 30.11, Kampuni ya Kutengeneza Nguzo za Zege Tanzania Sh. milioni 23.63, Chuo Kikuu cha Ardhi Sh. milioni 22.32, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) Sh. milioni 15.79, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tanga Sh. milioni 11.78 17 na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Korogwe Sh. milioni 11.26.

**SHIDA TANESCO**

CAG pia anasema TANESCO inakabiliwa na tatizo la kuchelewa utatuzi wa migogoro mitatu inayohusiana na tozo za Kampuni ya Songas Sh. bilioni 109.07 ambapo Oktoba 11, 2001, walitia saini mkataba wa ununuzi wa umeme wa miaka 20.

Anasema utekelezaji wa mikataba na mwenendo wa malipo unaonesha kuwapo mizozo endelevu ambayo haijatatuliwa tangu mwaka 2022 na kuwa shirika hilo lililipa malipo hayo yanayofikia Sh. bilioni 67.94.

# Shida yaibuliwa ujenzi Daraja la Nyerere

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini malimbikizo ya riba ya Sh. bilioni 103.22 yaliyotokana na kushindwa kulipa madai ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ya ujenzi wa daraja la Nyerere (Kigamboni).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2022/23 iliyowasilishwa bungeni juzi, CAG Charles Kichere anabainisha kuwa Novemba 20, 2014, Wizara ya Ujenzi iliingia mkataba na Bodi ya Wadhamini ya Mfuko huo kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa daraja hilo na barabara zake mkoani Dar es Salaam.

Gharama zote za mradi zilikuwa Dola za Marekani milioni 143.50 sawa na Sh. bilioni 238.71 (zilizorekebishwa mwaka 2016 hadi kufikia Sh. bilioni 328.9).

Kwa mujibu wa ibara za 2, 4, na 5 za mkataba, NSSF ilitakiwa kuchangia asilimia 60 ya gharama za mradi huku serikali ikitakiwa kuchangia asilimia 40.

CAG anasema michango kutoka kwa kila upande ilipaswa kutolewa kwa kuzingatia madai ya kazi zilizokamilika, huku riba ikitozwa kwa ucheleweshaji malipo baada ya siku 90 kulingana na kiwango cha riba cha Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Pia NSSF ilipewa haki za usimamizi wa daraja hilo kwa miaka 30 baada ya ujenzi, ikijumuisha ukusanyaji ushuru wa magari na pikipiki zinazovuka daraja hilo ili kurejesha uwekezaji wake.

CAG anasema kuwa kutokana na upungufu wa fedha serikalini, NSSF ilitoa gharama zote za mradi na serikali ilikubali kurejeshea mfuko huo Sh. bilioni 215.03, ikijumuisha gharama za ulipaji fidia wa eneo la ujenzi Sh. bilioni 14.14; asilimia 40 sawa na Sh. bilioni 124.54 ya mchango wa serikali katika mradi pamoja na riba ya Sh. bilioni 76.34 hadi Juni 30, 2021.

Hata hivyo, anasema hadi kufikia Juni 30, 2023, serikali haikuulipa mfuko huo gharama za mradi wa Sh. bilioni 215.03, hivyo kusababisha riba iliyotokana na ucheleweshaji huo wa malipo kuongezeka kutoka Sh. bilioni 76.34 Juni 30, 2021 hadi Sh. bilioni 103.22 Juni 30, 2023.

CAG anasema aliambiwa sababu kubwa ya kuchelewa kulipa madeni ya mfuko huo ni kutotolewa kwa fedha na Wizara ya Fedha.

"Hivyo, ucheleweshaji huo wa malipo kwa mfuko unaweza kuhatarisha hali ya kifedha ya mfuko na kusababisha ucheleweshaji malipo ya pensheni kwa wastaafu.

"Ucheleweshaji huu wa malipo ya pensheni unaweza kuathiri vibaya ustawi na ubora wa maisha ya wastaafu na wategemezi wao," CAG anahadharisha.

Mdhibiti anapendekeza serikali kuhakikisha malipo ya fidia ya madai ya NSSF kwa mradi wa Daraja la Nyerere yanafanyika ili kulinda utulivu wa mfuko wa pensheni.

### MIKOPO CHECHEFU

CAG pia ameonesha hasara inayotarajiwa ya Sh. bilioni 20.43 kwenye mikopo chechefu kutokana na kushindwa kufanya marejesho ya mikopo.

Katika ukaguzi wake kwenye Mfuko wa Pembejeo za Kilimo (AGITF), CAG amebaini mfuko ulikuwa na mikopo ambayo ilikuwa haijarejeshwa yenye thamani ya Sh. bilioni 25.42 hadi Juni 30, 2023.

Kati ya mikopo hiyo, mfuko ulitenga kiasi cha hasara tarajiwa kutokana na wakopaji kushindwa kurejesha mikopo jumla ya Sh. bilioni 20.43, ikiashiria matarajio ya kupata hasara ya takribani asilimia 80 ya mikopo iliyotolewa.

CAG anasema mfuko ulitarajia hasara ya asilimia 100 kwenye mikopo ambayo ilikuwa haijarejeshwa kwa muda wa siku 721, ambayo ni jumla ya Sh. bilioni 19.83. Kwa mikopo iliyobaki ya Sh. milioni 600, mfuko ulitarajia hasara ya kati ya asilimia moja hadi 50.

Vilevile, CAG anabainisha kuwa kati ya mikopo ambayo haikurejeshwa, Sh. bilioni 1.71 ni mikopo ambayo haikurejeshwa kuanzia mwaka 1995 hadi 1997, ikionesha ucheleweshaji wa kati ya miaka 26 na 28.

Pia inajumuisha mikopo ya jumla ya Sh. milioni 801.38 iliyotolewa kwa benki nne zilizofungwa na BoT kati ya mwaka 2017 na 2018.



Rundo la taka likiwa limetelekezwa bila ya kuzolewa pembeni ya kituo cha daladala cha Gongo la Mboto, jijini Dar es Salaam jana na kusababisha kero na harufu mbaya kwa abiria na wafanyabiashara wa eneo hilo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Akaunti zenye Dola zabainika hazijaguswa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) amebaini kuwapo akaunti za benki ambazo hazijatumika kwa zaidi ya mwaka mmoja amezitaja ni za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA), hali inayohatarisha serikali kupata hasara ya mamilioni ya shilingi.

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2022/23, CAG Kichere anasema amebaini TAA ilikuwa inamiliki akaunti tatu za benki ambazo hazikutumika kwa zaidi ya mwaka mmoja ambapo hadi Juni 30, 2023, zilikuwa na kiasi cha dola za Marekani 209 pamoja na Sh. milioni 170.14.

Vilevile, CAG anasema amebaini TBA pia ilikuwa na akaunti dumavu 33 za benki ambazo hazikuwa zinatumika tangu mwezi Oktoba 2020 na kati ya akaunti hizo, saba zilikuwa na kiasi cha Sh. milioni 12.48 hadi Juni 30, 2023.

"Kwa maoni yangu, upungufu huu unadhihirisha usimamizi mdogo wa akaunti za benki, hali ambayo kwa upande mwingine, inaweza kuiweka serikali katika hatari ya kupata hasara za kifedha, matumizi mabaya ya fedha za umma na kuruhusu mianya ya ubadhirifu.

"Ninapendekeza serikali kwa kushirikiana na TAA na TBA pamoja na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, ifunge akaunti zote zisizotumika ili kupunguza hatari ya hasara za fedha, matumizi mabaya ya fedha za umma na hatari ya shughuli za udanganyifu.

"Pia ninapendekeza serikali kuhakikisha TAA inaimarisha usimamizi wa miundombinu ya viwanja vya ndege na kuzingatia kanuni na hatua za usalama ili kulinda usalama wa wafanyakazi, abiria na uendeshaji wa viwanja vya ndege," CAG anawasilisha hoja yake.

### TAA 217 ZATELEKEZWA

CAG pia amebaini taa 217 za uwanja wa ndege (AGL) zenye thamani ya Dola za Marekani 334,986.05 katika Uwanja wa Ndege wa Dodoma zinazotumia nishati ya jua zilitelekezwa kwenye stoo ya uwanja huo baada ya kubadilishwa na uwanja kuanza kutumia taa zinazotumia nishati ya umeme.

Anaonesha wasiwasi hali ya taa hizo zilizotelekezwa inaweza kuwa mbaya kutokana mambo mbalimbali kama vile ukosefu wa matengenezo na uharibifu unaoweza kutokea kutokana na utunzaji usioridhisha.

### SIMU ZAONGOZA NDEGE

Vilevile, CAG anasema amebaini kwenye Uwanja wa Ndege Bukoba, wafanyakazi wa udhibiti wa ndege ardhini walikuwa wanatumia simu za mkononi kupokea taarifa za safari na kuwasiliana na Mnara wa Udhibiti wa Ndege ulioko Mwanza, jambo ambalo ni kinyume cha sheria.

# JKCI kufikisha tiba ya moyo mikoa yote

**Na Joseph Mwendapole**

TAASISI ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) imeahidi kuifikia mikoa yote nchini kusogeza huduma za kibingwa za matibabu ya moyo kwa wananchi kupitia kambi maalumu za uchunguzi na matibabu.

Hayo yalisemwa jana mkoani Iringa na Mkuu wa Kitengo cha Mafunzo na Utafiti wa JKCI, Dk. Pedro Pallangyo, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kabla ya kuanza kwa kambi maalumu ya matibabu ya moyo ijulikanayo kama Dk. Samia Suluhu Hassan Tiba Mkoba.

"Kupitia huduma hii ya tiba ya Dk. Samia Suluhu Hassan, JKCI imeweza kufikia mikoa 13 na kuwahudumia wananchi 11,254", alisema Dk. Palanyo.

Alisema huu ni mwaka wa pili mfululizo JKCI inafanya kambi maalumu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Iringa (IRRH) kwa lengo la kuweka nguvu ya pamoja kuhudumia jamii ya Watanzania wanaohitaji huduma za kibingwa za matibabu ya moyo.

Dk. Pallangyo alisema Tanzania ni kubwa na JKCI ndio taasisi pekee ya serikali ya kibingwa ya matibabu ya moyo, hivyo wananchi wote hawawezi kuifikia taasisi hiyo mahali ilipo.

"Tunapokuja katika kambi kama hii tunafahamu siku tano hazitoshi lakini tunaweza kutoa huduma kwa kiwango kile tulichotegemea kufanya angalau wale waliokuwa hawana uwezo wa kusafiri wanapatiwa huduma", alisema.

HABARI KITAIFA

# TAMISEMI yataja vipaumbele

**Na Vitus Audax,** DODOMA

WIZARA ya Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imeweka sura ya bajeti ya makadirio ya mapato na matumizi 2024/25 ya Sh. trilioni 10.125 na kutoa vipaumbele katika Elimu, Afya na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

**ELIMU**

Imepanga kutumia Sh. trilioni 1.02 kupitia ruzuku ya Serikali Kuu na washirika wa maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli katika sekta ya elimu katika usimamizi, uendeshaji wa elimu msingi na sekondari.

Mchengerwa (pichani) alitaja shughuli zitakazotekelezwa kuwa ni pamoja na ujenzi wa vyumba vya madarasa 6,357, matundu ya vyoo 1,482, umaliziaji wa mabwalo 362 kati ya hayo 15 ni msingi na 347 ni ya sekondari na umaliziaji mabweni 36 kwenye shule za awali na msingi.

Pia, alitaja ujenzi wa shule mpya 184, nyumba za walimu 184 na mabweni 186 katika shule za sekondari, ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwenye shule za awali tatu, msingi 400 na sekondari 500.

Alitaja ununuzi wa kemikali za maabara katika shule mpya 234, utoaji wa ruzuku ya elimu bila ada kwa shule za msingi 17,986 na sekondari 4,894; ununuzi na usambazaji wa vitabu 2,215,877 kwa shule za msingi na 11,880,828 kwa shule za sekondari pamoja na vitabu na vifaa vilivyoboreshwa vya kufundishia na kujifunzia elimu ya awali kwenye shule 4,500 pamoja na ununuzi wa vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika shule 130 za msingi na sekondari.



Kadhalika, kutoa mafunzo ya maadili kwa wakuu wa shule 17,220, viongozi na watumishi wa TSC 460 katika ngazi ya wizara na wilaya, kutoa mafunzo endelevu ya walimu kazini (MEWAKA) kwenye shule za awali na msingi kwenye halmashauri 140, kutekeleza mpango wa shule salama kwenye shule za awali na msingi 2,500.

Aidha, alisema serikali itaanzisha madarasa janja 10 kwa ajili ya ufundishaji mubashara katika halmashauri 10 yatakayosaidia kupunguza tatizo la uhaba wa walimu hususani katika masomo ya hesabu na sayansi.

**MIUNDOMBINU**

Katika sekta ya ujenzi alisema serikali inatarajia kutumia Sh. bilioni 841.19 kwaajili ya ujenzi, matengenezo, ukarabati wa miundombinu ya barabara, usafiri na usafirishaji wa vijijini na mijini.

Kati ya fedha hizo Sh. bilioni 257.03 ni za Mfuko wa Barabara, Sh. bilioni 127.50, Mfuko Mkuu wa Serikali, Sh. bilioni 325.77 ni za tozo ya mafuta ya petroli na dizeli ya Sh. 100 kwa lita, Sh. bilioni 4.03 za mapato ya ndani kupitia Wakala ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam na Sh. bilioni 126.85 ni fedha za nje.

Katika utekelezaji huo yanatarajiwa kufanyika matengenezo ya barabara za vijijini na mijini zenye urefu wa kilomita 20,745.31, ujenzi wa barabara za lami zenye urefu wa kilomita 434.50, ujenzi wa barabara za changarawe zenye urefu wa kilomita 13,802.34, ujenzi wa madaraja 160 na ukarabati wa madaraja.

Shughuli nyingine ni ujenzi na matengenezo ya boksi kalavati 586 na vivuko 15, ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua yenye urefu wa mita 141,070.54, ujenzi wa kingo za Mto Msimbazi, kudhibiti maeneo ya juu ya Mto MsimbAlitaja ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilomita 250, kupitia mradi wa uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam awamu ya pili na kati ya hizo kilomita 132 zimefanyiwa usanifu.




Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akifungua kikao cha kujadili changamoto za mabadiliko ya tabianchi yanayoikumba Dunia na utatuzi wake, wakati wa Mkutano wa Mwaka wa Jukwaa la Kibunge la Benki ya Dunia na Shirika la Fedha Duniani, Washington DC, nchini Marekani jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# EPZA: Wawekezaji changamkieni fursa

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA) imewataka wawekezaji wa ndani na nje kuchangamkia fursa ya uwekezaji kwenye uzalishaji wa vipuri vya magari na mitambo mbalimbali hatua itakayowezesha kupambana na uingizaji feki kutoka nje ya nchi.

Hayo yamesemwa na Ofisa Uhamasishaji wa Mamlaka ya EPZA, Blandina Mwasamwene wakati wa ziara ya ufuatiliaji na tathmini ya viwanda vilivyopatiwa leseni na EPZA kuwekeza kwenye Maeneo Maalum ya Uwekezaji kwa mauzo nje (EPZ) na Maeneo Maalum ya kiuchumi (SEZ) katika mkoa wa Dar es Salaam hivi karibuni.

"Kuna fursa kubwa sana katika sekta ya magari na hasa kwenye uzalishaji wa vipuri vya viwanda ambapo wenye magari wengi wanaagiza nje ya nchi," alisema.

Mamlaka ya EPZA inatoa leseni na vivutio mbalimbali kwa wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza katika maeneo ya EPZ na SEZ.

Naye Mkurugenzi wa kiwanda cha kutengeneza vipuri vya magari cha Spincast Engineering, Yusuph Khalfan, ambacho kimepewa leseni na EPZA, alisema kiwanda hicho kinachomilikiwa kwa asilimia 100 na Watanzania, kinatumia teknolojia ya kisasa kutengeneza vipuri vyenye ubora kama vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi.

Alisema kuwa pia wana mtambo wa kisasa ambao unashughulika na uzalisha na vifaa kwa ajili ya mitambo mbalimbali na magari.

Alisema kiwanda hicho ambacho kimeajiri watu zaidi ya 20 wote wakiwa Watanzania, pia kinatoa mafunzo kuwaendeleza vijana namna ya kuendesha mitambo hiyo ya kisasa kwa ajili ya kutengeneza vifaa hii vya magari na mitambo.

Kwa mfano kwa sasa tunatengeneza cylinder liners ambazo zinakuwa na viwango vya kisasa ikilinganishwa na vinavyotoka nje ya nchi.

Alisema wenye magari kwa sasa wanapendelea kununua vifaa kutoka kwa kutokana na urahisi wa upatikanaji wake na uhakika wa ubora.

Alisema kiwanda pia hutengeneza vipuri mbalimbali kutokana na mahitaji ya mteja ambavyo vinakuwa na ubora wa hali ya juu kulinganisha na vile kutoka nje ya nchi.

Alisema zaidi ya soko la ndani, pia wataangalia soko la Afrika hasa nchi za Afrika Kusini, Nigeria, Zambia na Kongo.

Ofisa wa Utawala na Rasilimali Watu wa kiwanda cha SB Plastics EPZ Limited, Gabriel Richard, ambacho kilitembelewa pia na maofisa wa EPZA, alisema kiwanda hicho kinachojishughulisha na kuchakata chupa tupu kimeanzishwa mwaka 2013.


## NOTISI YA SIKU 14/ TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**HARVESTER CAPITAL INVESTMENT** Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na **MWANGA HAKIKA BANK LIMITED,** tutauza kwa njia ya Mnada wa hadhara mali/dhamana za wadaiwa wake kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utafanyika mahali dhamana zilipo baada ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya Notisi /Tangazo hili endapo hawatalipa madeni yao.

| NA | JINA LA MDAIWA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE NA SAA YA MNADA | KAMPUNI/DALALI HUSIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | FLORA ANDREA KIDIKA | FLORA ANDREA KIDIKA | KIWANJA KILICHPO LOSIRWAI | KIWANJA KIPO LOSIRWAI, KATA YA MUSHONO, WILAYA YA ARUSHA | 02/05/2024 SAA 03:30 ASUBUHI NA KUENDELEA | HARVESTER CAPITAL INVESTMENT |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi wa dhamana unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Mali/dhamana itauzwa katika hali ilivyo na mahali ilipo.
3. Mshindii wa mnada atalazimika kulipa malipo yasiyopungua 25% ya bei iliyofikiwa siku yamnada, na 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa na bank (eviction) ni za mnunuzi.
5. Mnunuzi akishindwa kutimiza sharti moja wapo hapo juu malipo ya awali hayatarejeshwa na mnada utarudiwa.

**HARVESTER CAPITAL INVESTMENT**
**P.o.Box 11898**
**Arusha**
**Tel: 0784 200283/ 0767529605**
**Email: harvestercapital558@gmail.com**
**Kwa maelezo zaidi wasiliana na:**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usimamizi unatakiwa mikopo ya asilimia 10

**SERIKALI** jana ilitangaza kuanza utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kuanzia Julai, mwaka huu, kwa kutumia utaratibu mpya wa kupitia benki. Katika kuanza utaratibu huo mpya wa mikopo, mamlaka 10 za serikali za mitaa zitaanza kama maeneo ya majaribio.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2024/25 bungeni jana, alisema mfumo huo wa utoaji mikopo umeboreshwa baada ya kubaini upungufu katika mikopo ya awali.

Mchengerwa alizitaja halmashauri zilizoteuliwa kuanzia utoaji mikopo hiyo kwa majaribio ni majiji ya Dar es Salaam na Dodoma, manispaa za Kigoma Ujiji na Songea, halmashauri za miji za Newala na Mbulu na wilaya za Siha, Nkasi, Itilima na Bumbuli. Kuhusu halmashauri 174 zilizobaki.

Ni dhahiri kwamba uteuzi wa halmashauri hizo umezingatia tofauti za kimifumo katika uendeshaji na jiografia ya mahali zilipo.

Sambamba na utaratibu wa utoaji mikopo kupitia benki, Waziri Mchengerwa alisema maboresho yanatarajiwa kufanyika ikiwamo uanzishwaji wa kitengo cha usimamizi wa mikopo hiyo katika OR-TAMISEMI na uanzishwaji wa kamati za usimamizi katika ofisi za wakuu wa mikoa, halmashauri na kata.

Katika ngazi ya kata, alisema kamati zitakuwa na majukumu ya kutambua waombaji na kuthibitisha vikundi vya mikopo na kuvisajili kwenye mfumo kabla ya kuwasilisha kwenye kamati ya halmashauri.

Kazi zingine zilizofanyika katika uboreshaji wa mfumo mpya ni pamoja na kusanifu na kujenga mfumo mpya unaoitwa 'Wezesha Portal' utakaotumika kwa ajili ya taratibu za ukopeshwaji wa makundi husika. Hatua hiyo pia itaondoa changamoto za mfumo zilizokuwapo awali kabla ya mikopo kusimamishwa.

Jambo lingine linaloonyesha kwamba mfumo huo mpya umeandaliwa vyema ili kuondoa kasoro zilizokuwapo awali ni kuwapo kwa mpango wa kuwajengea uwezo wasimamizi wa mikopo kwa kuwapa mafunzo na pia kuongeza idadi ya wasimamizi wa mikopo kwenye ngazi ya kata kwa kuajiri maofisa maendeleo ya jamii 787 na kupangiwa kata zilizokuwa na upungufu.

Katika kuhakikisha kunakuwa na ufanisi, serikali imepanga kurekebisha sheria inayosimamia mikopo hiyo na kanuni zake na baada ya kipindi cha mpito, tathmini itafanyika ili kubaini mfumo bora utakaotumika katika utoaji wa mikopo hiyo.


Hatua ya kurejeshwa kwa mikopo hiyo inatokana na serikali kutambua umuhimu wake katika kuyakwamua makundi maalumu kutoka katika utegemezi na umaskini ili kuwa na uchumi na maisha bora. Kutokana na umuhimu huo, Sh. bilioni 227.96 zikiwamo Sh. bilioni 63.67 ambazo ni za marejesho ya fedha zilizokuwa zikidaiwa kukusanywa kutokana na mikopo iliyotolewa kabla ya kusimamishwa.

Hata hivyo, kwa kipindi kirefu kumekuwa na taarifa za Mdhibiti na Mkaguzo Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu kutafunwa kwa mabilioni yas fedha katika serikali kuu na taasisi zake, mamlaka za serikali za mitaa zikiwamo.

Kutokana na hali hiyo, ni vyema udhibiti na umakini katika usimamizi wa mikopo hiyo vikafanyika ili kuziba matundu ya upotevu wa mamilioni. Hata mikoa iliyositishwa kulikuwa na ubadhirifu na udanganyifu mwingi kutokana na baadhi ya viongozi kujinufaisha kwa kutumia vikundi hewa.

Kwa mfumo mpya, ni imani kwamba serikali imejifunza kutokana na makosa yaliyopita ndiyo maana imeandaa mikakati kabambe katika kuziba mianya kwa kuweka mifumo na kamati za utambuzi hadi ngazi ya kata.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wanasheria tusaidieni kutatua mkanganyiko jina Tume Uchaguzi

Na Sabato Kasika

**KUANZIA** Aprili 12 mwaka huu, iliyokuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imebadilishwa jina na kuwa Tume Huru ya Uchaguzi, ni baada ya kukamilika kwa mabadiliko ya sheria ya tume ya taifa ya uchaguzi.

Hata hivyo, hatua ya serikali kutangaza jina jipya la tume hiyo, imezua mjadala miongoni mwa wadau, hasa viongozi wa vyama vya siasa wanatamani mabadiliko ya jina hilo yaambatane na mabadiliko ya Katiba.

Kinachoguswa ni Sheria Na. 2 ya mwaka 2024 ambayo ni kati ya sheria tatu zilizotiwa saini na Rais Samia Suluhu Hassan, ikiwamo ya uchaguzi wa Rais, wabunge na madiwani ya mwaka 2024.

Nyingine ni Sheria ya Vyama vya Siasa ya mwaka 2024. Tangu kutungwa sheria hizo hadi kupitishwa kwake, kumekuwapo na mjadala ambao sasa unazidi kupamba moto baada ya jina la tume kubadilishwa.

Wapo wanaosema hawakubaliani na kuundwa kwa tume hiyo bila kubadilisha katiba ya nchi. Wengine wanasema,jambo la msingi si kubadili jina la tume bali kufuata matakwa ya sheria mpya ya Tume ya Uchaguzi ya Mwaka 2024 iliyobadili jina la tume.

Kwa ujumla ni kwamba, vyama vya siasa vinaonekana kupishana katika mchakato mzima wa sheria tatu mpya za uchaguzi zilizosainiwa na Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, Machi 29 mwaka huu.

Mkanganyiko wa tume hiyo unatajwa na wadau kuwa uko kwenye vigezo, kuanzia jinsi itakavyofanya kazi, uwezo wake kifedha, ilivyoundwa kisheria na aina ya watu wanaoongoza na weledi wao.

Kwa kuwa kumekuwapo na mjadala mpana baada ya jina jipya kutangazwa, ninadhani ni wakati sasa kwa wanasheria kujitokeza na kutoa ufafanuzi wa kina ili kuwaweka sawa wadau.

> **Wanaamini kwamba tume za uchaguzi katika nchi nyingi za Afrika kufananisha uhuru na utendaji wa tume za uchaguzi za nchi hizo ni jambo lenye changamoto, kwa madai kwamba zinaingiliwa.**

Ninashauri hivyo kwa sababu, baadhi ya wadau wanaamini kuwa hilo ni jina tu na kwamba tume hiyo sio, kwa maelezo kuwa wajumbe wake ni walewale na pia mchakato wa kuwapata ni uleule wa zamani.

Wanaamini kwamba kwa mazingira hayo, hakutakuwa na uchaguzi huru na haki, badala yake limepachikwa jina la tume huru lakini ndani yake hakuna uhuru kama ambavyo wadau wamekuwa wakitamani.

Kwa kuwa hayo ni mambo ya kisheria, ni vyema wanasheria wakachambua na kuweka wazi kuhusu kile ambacho wadau hao wamekuwa wakijadili tangu kutangazwa kwa mabadiliko hayo.

Katika maelezo yao, wanaamini kuwa tume haina watumishi wake nchi nzima na kwamba inatumia wakurugenzi wa halmashauri kusimamia uchaguzi, na wadai kuwa wengi wakurugenzi hao ni makada wa CCM.

Wanaamini kwamba tume za uchaguzi katika nchi nyingi za Afrika kufananisha uhuru na utendaji wa tume za uchaguzi za nchi hizo ni jambo lenye changamoto, kwa madai kwamba zinaingiliwa.

Hivyo, kwa kuwa utata wa aina hiyo unaweza kutatuliwa na wataalam wa sheria, ambao watadadavua kwa kina ili uhuru wa tume ujulikane na kuwaondolea mashaka wadau wanaosema kilichobadilika ni jina tu.

Na ikiangaliwa hilo kwa kina, ni wazi huo ni wajibu wa kisomi kama alivyofafanua Mwalimu Julius Nyerere katika nadharia ya Elimu ya Kujitegemea, kwamba wasomi wanapoona kuna kigumu kinachohitaji huduma yao, wawe wa kwanza kuusaidia umma.

Sasa katika hilo, enyi wanasheria lipo mbele yenu, mnatakiwa kuwajibika, maana ndio weledi katika eneo hilo mkibeba tafsiri pana.

## TANESCO yatimua watano kwa rushwa

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

WATU watano waliokuwa wakifanyakazi na Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) mkoa wa Morogoro, wamefukuzwa kazi na kikundi chao kufutwa baada ya kubainika kujihusisha na vitendo vya rushwa.

Akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa, Meneja wa TANESCO Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Fadhili Chilombe, alisema watu hao ni kutoka kikundi cha Mlimba Constructions.

Aliwataja watu hao kuwa ni Majaliwa Mtasiwa, Lewis Isack, Ezekiel Myinga, Petro Mahenge na Stanley Mussa ambao wanatokana na jamii kupitia vikundi vyao na waliokuwa wakifanya kazi TANESCO lakini si waajiriwa.

"Tulikuwa tukiwapa kazi za 'survey' au kuwaunganishia umeme wateja, wanakwenda na kuomba fedha ya mafuta, mara chakula na wamefanya hivyo kwa muda mrefu na kusababisha malalamiko kwa wananchi," alisema.

Pia aliwataka wananchi wasikubali kuwapa kazi watu hao na wakiwagundua wanataka kufanya kazi za TANESCO, watoe taarifa kwenye ofisi za serikali katika maeneo yao, polisi, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) au kwa meneja ili wakamatwe na kuchukuliwa hatua zaidi.

"Kama hawa tuliowafukuza, zilikuwa kelele za muda mrefu na mara ya mwisho wametengeneza 'link' (mtandao) ya kupata hela kwa mteja na wakaomba Sh. 800,000 na zilishatolewa. Walipobanwa walirudisha," alisema Chilombe.

Aliwaambia wananchi kuwa baada ya kufunga nyaya (wiring) kwenye nyumba, wanapokwenda kuchukua fomu ya maombi ya umeme ni bure na kuunganisha umeme vijijini ni Sh. 27,000 na mjini ni kuanzia 321,000. Alisema gharama itaongezeka kutegemeana na umbali atakaohitaji nguzo na kwamba fedha zingine zinazoombwa na kwamba majina mbalimbali ni rushwa na waziripoti.

Pia alisema hata hitilafu za umeme ambazo mafundi binafsi watawaeleza wateja kuwa si za ndani ya nyumba bali za nje, zinazopaswa kurekebishwa na TANESCO, kazi ambayo hufanywa bure.

Alisema hatua za kuwakamata watuhumiwa wa rushwa ndani ya shirika hilo ni maelekezo yaliyotolewa na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Dotto Biteko, hivi Karibuni ili kurudisha heshima ya shirika.



Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Kata ya Kipunguni, jijini Dar es Salaam, Rozina Soka, akifungua mkutano wa wajasiriamali wanawake wa kata hiyo juzi, uliojadili fursa mbalimbali za mikopo ikiwamo ya asilimia kumi inayotolewa na halmashauri. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Mwalimu achanja mbuga wadai walipomvaa shuleni

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WANAFUNZI wa Shule ya Msingi Luwa katika Manispaa ya Sumbawanga mkoani Rukwa, juzi walikatisha masomo kwa takribani saa tatu baada ya wajasiliamali kufika shuleni hapo na kumfanyia shambulio la aibu Mwalimu Mkuu wa Shule kwa madai ya kushinikiza walipwe fedha wanazomdai mwalimu aliyekopa bidhaa kwao.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii, Mwenyekiti wa Kijiji, Stedius Pastory, alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 3 asubuhi wakati mwalimu waliyekuwa wakimdai akiwa shuleni hapo akiendelea na majukumu yake.

Alisema mwalimu aliyedaiwa baada ya kuwaona wajasiriamali hao wakifika shuleni hapo na gari lao, ghafla alitimua mbio na kukimbilia kwenye shamba la mahindi karibu na shule hiyo ndipo mmoja kati yao alianza kumkimbiza.

"Baada ya kushindwa kumkamata, alirejea katika eneo la shule na kuungana na mwenzake aliyekuwa amebaki kwenye gari na kwenda moja kwa moja walimvamia ia mwalimu mkuu aliyekuwa akizungumza na wazazi wa wanafunzi waliokuwa wamefika kulipa michango kisha kumkaba, kumkatia vishikizo vya shati na kupasua simu janja yake.

Wakati wajasiliamali hao wakifanya vitendo hivyo, wazazi waliokuwapo eneo hilo waliwakamata na kuwazuia wajasiliamali hao ndipo mwalimu mkuu alipokimbilia ofisini kwake na kujifungia ili kujinusuru na hasira za watu hao.

"Wazazi hao walipowaachia wafanyabiashara hao, walichukua mawe na kuanza kuponda mlango wa ofisi ambayo mwalimu mkuu alijificha na pia kukatakata matawi ya miti iliyoko shuleni hapo kwa hasira huku wakiwa kama wamepandisha kichaa kwa madai kuwa wanataka kulipwa fedha zao," alisema mwenyekiti wa kijiji.

Alisema wanafunzi waliokuwa madarasani walikuwa wakishuhudia vurugu zinazotokea na baadhi yao walikimbilia kijijini kwenda kuwaita wazazi wao ili wakamsaidia mwalimu mkuu kwa kuwa waliona anapigwa na wafanyabishara hao waliovamia shule yao.

Kundi la wazazi lilifika shuleni hapo baadhi wakiwa na silaha za jadi ndipo wajasiliamali hao walipopanda gari lao na kuondoka katika eneo la shule na kutimkia kusikojulikana.

Mwenyekiti Pastory alisema mwalimu aliyekuwa anadaiwa alikopa redio, televisheni na vyombo mbalimbali vya ndani na alikuwa akisumbua kulipa na wakati mwingine alikuwa akiwakimbia wafanyabiashara hao kitendo kilichowapa hasira na kuamua kufanya vurugu shuleni hapo.

Mwenyekiti wa Chama cha Walimu (CWT) Manispaa ya Sumbawanga, Mwalimu Huruma Kilingo, aliwashauri walimu kuacha tabia za kukopa wakati wanajua hawana uwezo wa kulipa kwa kuwa vitendo kama hivyo vinaharibu haiba yao.

Pia alisema kwa mujibu wa sheria za utumishi ni makosa kufanya biashara katika maeneo ya shule na kitendo kilichofanyika kinapaswa sheria zichukuliwe ili kukomesha biashara katika maeneo hayo kwa kuwa wanawakosesha wanafunzi haki ya kupata masomo.

**KABWELA** Na Fadhil Mohammed



# Bil. 216/- kugharamia chanjo mifugo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeandaa programu ya uchanjaji mifugo dhidi ya magonjwa ya kipaumbele ya miaka mitano ambayo itagharimu Sh. bilioni 216.

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Alexander Mnyeti, alitoa kauli hiyo juzi bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Igalula (CCM), Venant Protas.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji kwa nini serikali isitoe elimu pamoja na chanjo bure kwa wafugaji wa ng'ombe nchini.

Akijibu swali hilo, Mnyeti alisema hali ya uchanjaji kwa sasa ipo chini ya asilimia 50 ambayo ni chini ya malengo ya kuchanja mifugo kwa angalau asilimia 70 kwa kila ugonjwa unaolengwa.

"Ili kuhakikisha utoaji chanjo unafikia asilimia 70 inayolengwa, Wizara imeandaa programu ya uchanjaji mifugo dhidi ya magonjwa ya kipaumbele ya miaka mitano ambayo itagharimu Sh. bilioni 216,"alisema.

Pia alisema programu hiyo itaanza kutekelezwa katika bajeti ya mwaka 2024/25 ambapo kiasi cha Sh.bilioni 29 kimetengwa kwa ajili ya kuanza kampeni ya utoaji wa chanjo ya ruzuku dhidi ya magonjwa ya mifugo ya kipaumbele.

Alisema Wizara imeendelea kutoa elimu ya umuhimu wa chanjo kupitia vyombo vya habari, maonesho mbalimbali yakiwamo maonesho ya nanenane, sabasaba, programu mbalimballi za utoaji elimu kwa umma na mafunzo rejea kwa wataalamu wa mifugo.

Mnyeti alisema mamlaka za serikali za mitaa kupitia wataalam wa mifugo zimeendelea kutoa elimu bure kwa wafugaji juu ya umhimu wa chanjo na uchanjaji wa mifugo.

Alisema katika kuhakikisha wafugaji wanachanja mifugo yao, wizara iliandaa kanuni za chanjo na utoaji wa chanjo kwa mwaka 2020 ambazo zinamtaka mfugaji kuchanja mifugo yake kuendana na kalenda ya uchanjaji wa magonjwa ya mifugo.



Meneja wa kampuni ya Uchapishaji ya Mkuki na Nyota,Tapiwa Muchechemera (kushoto), akikabidhi msaada wa vitabu vya aina mbalimbali kwa Mwanzilishi wa maktaba ya kijamii ya Martha Onesmo ya wilayani Mwanga, mkoani Kilimanjaro, Jennifer Dickson katika hafla fupi, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi SUA wafundwa kuhusu malengo

**Na Munir Shemweta,** MLELE

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Kampasi ya Mizengo Pinda, Mpimbwe wilaya ya Mlele mkoani Katavi wametakiwa kusoma kwa bidii na malengo ili wapate kile walichokusudia kukipata.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mbunge wa Kavuu, Geophrey Pinda, alisema hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na wanafunzi hao kwa lengo la kujua changamoto zinazowakabili.

Alisema ni vyema wanafunzi wanaosoma katika chuo kikuu hicho Kampasi ya Mizengo Pinda, wakarejea na kuangalia malengo yaliyowapeleka sambamba na yale ya wazazi wao ili kupata kile wanachohitaji kutoka chuo hapo.

"Kama umekubali kuja katika chuo cha Katavi ambacho kiko mbali na macho yaliyo wazi na umekubali kuja hapa kuwa 'serious' na masomo yako, utapata kitu kikubwa sana," alisema Pinda.

Wanafunzi wa chuo hicho mbali na kumshukuru Mbunge kwa kuwatembelea ili kujua changamoto zinazowakabili, walimwomba kuwasaidia kutatua changamoto mbalimbali chuoni hapo ikiwamo kupatiwa mizinga ya nyuki kwa ajili ya masomo ya vitendo, mipira kwa ajili ya mpira wa niguu na pete pamoja na televisheni.

Pia walimwomba kusaidia upatikanaji mikopo kwa wanafunzi wasiopata mikopo ya elimu ya juu. Walisema pamoja na mikopo kupatikana kwa asilimia tofauti kwa wanafunzi wa chuo hicho, bado kuna baadhi yao hawakupata kabisa jambo linalowafanya kuishi kwa shida.

"Ukiangalia mtu hana uwezo na mfano ni kwa mmoja wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza katika chuo chetu wakati mwingine inatulazimu sisi wanafunzi wenzake timchangie" Wamesema wanafunzi.

"Hapa kuna wanafunzi wa mwaka wa kwanza hawajapata mikopo ya elimu ya juu na yupo mmoja ukimuangalia hana uwezo kabisa tulilazimika kumchangia fedha," walisema.

Naibu RASI wa Ndaki Taaluma Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Kampasi ya Mizengo Pinda, Prof. Anna Sikila, alisema mazingira mazuri ya chuo yamewafanya wanafunzi kusoma vizuri na kujituma katika masomo.

Kwa mujibu wa Profesa Sikila, kujituma na kusoma kwa bidii kwa wanafunzi wa chuo hicho kumesababisha mwaka jana mwanafunzi kuongoza kimasoma kwa kampasi zote za Mizengo Pinda na Kampasi Kuu ya SUA, Morogoro.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Kampasi ya Mizengo Pinda kinatoa kozi za Shahada ya Sayansi ya Usimamizi wa Rasilimali Nyuki, Stashahada ya Uzalishaji na Usimamizi wa Mazao pamoja na Astashahada ya Uongozaji Watalii na Uwindaji wa Kitalii.

## Polisi yazindua kampeni mpya kukabili uhalifu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Dodoma limezindua kampeni ya 'Familia Yangu Haina Mhalifu 2024' ambayo imeanza kwa shule za msingi ikilenga kutokomeza uhalifu.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika uzinduzi huo uliofanyika Shule ya Msingi Chadulu, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Theopista Mallya, alisema wameanza katika shule za msingi kwa imani kwamba watoto wadogo wakipewa elimu ni rahisi kuifanyia kazi.

"Hatuishii hapa bali tutakwenda kwenye nyumba za ibada ili kuwapa watu elimu kuhakikisha kama familia hazitakuwa na uhalifu basi mtaani hakutakuwa na uhalifu,"alisema.

Alisema jeshi hilo limejipanga kutoa elimu kwa kina kukabiliana na uhalifu kwenye familia.

"Kuna baadhi ya familia uhalifu unatendeka ndani na kama familia ipo kwenye mtaa kuna uhalifu basi kutakuwa hakuna amani wala usalama kwasababu hiyo familia itakuwa inasumbua mtaa, hivyo kuwatumia watoto wadogo watatuambia kama kwenye familia yao kuna wezi, wabakaji, walawiti, vipigo watuambie,"alisema.

Aliwataka watoto kuhakikisha familia zao hakuna uhalifu.

"Tutapambana na hao maharamia wanaolawiti na kubaka watoto, na niwaambie watu wa Dodoma nitaendelea kutoa elimu kwa makundi yote kinachotakiwa ni ushirikiano na jeshi la polisi ili kutokomeza uhalifu Dodoma,"alisema.

Kamanda huyo alisema ushirikiano kati ya jamii na jeshi hilo utasaidia kutokomeza hali hiyo.

"Watoe taarifa za uhalifu tutawalinda namba yangu ya simu ipo saa 24 piga simu mwananchi yeyote tutafanyia kazi taarifa zako, na usimsingizie mtu kwa atakayemsingizia mtu kwa mabifu yao tukikubaini tutakuchukulia hatua,"alisema.



# Askari Afrika Mashariki wajifua kukabiliana ugaidi, uhalifu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ASKARI polisi 561 kutoka nchi saba za Afrika ya Mashariki, wameanza kujifua namna ya kukabiliana na vitisho vya ugaidi na uhalifu unaovuka mipaka.

Mkazo zaidi katika mafunzo hayo umewekwa katika vita ya usafirishaji dawa za kulevya, binadamu, ujambazi na utoroshaji wa mifugo.

Tanzania imekuwa mwenyeji wa zoezi la mafunzo ya utayari kwa vitendo mwaka 2024 linalojumuisha nchi 14 wanachama wa Shirikisho la Wakuu wa Polisi Ukanda wa Mashariki mwa Afrika (EAPCCO) kati ya Aprili 14 hadi 19.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Dk. Maduhu Kazi, akifungua mafunzo hayo jana katika Shule ya Polisi Moshi na baadae kuzuru Viwanja vya Medani za Kivita Kilelepori, Wilaya ya Siha, alisema mambo mengine yatakayokuwa mkakati wa pamoja ni kuangalia namna ambavyo nchi hizo zinaweza kuwa na mianya ya kiusalama na kimipaka.

"Kikubwa sana ni suala la utayari wa masuala ya ugaidi na uhalifu unaovuka mipaka hua yanakuja bila kutarajia hasa masuala ya ugaidi. Kwa hivyo mafunzo yatakayotolewa hapa yanawaweka tayari vyombo vyetu vya polisi kukabiliana na masuala ya ugaidi," alisema.

Alisema pamoja na hayo, wanajifunza namna ambayo vitendo vya ugaidi na uhalifu wa kimataifa unavyofanyika lakini na magaidi wanavyopata fedha.

Alisema kuna masuala mengine ambayo watakuwa wakiangalia namna ambavyo nchi wanachama zinaweza kuwa na mianya ya kiusalama na kimipaka, ambayo inaweza kutokea na kuleta nafasi kwa wahalifu wakaweza kupenya na kuhatarisha maisha pamoja na hali za watu katika ukanda.

Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini (IGP), Michael Wambura, akizungumzia mafunzo hayo, alisema washiriki wake ni maofisa, wakaguzi na askari wa vyeo mbalimbali 561.

IGP Wambura alisema: "Kufanyika kwa zoezi hili kunatokana na maazimio ya wakuu wa EAPCCO katika mikutano yao ya kila mwaka. Nia yetu ni kuwajengea uwezo wa kubaini, kuzuia uhalifu unaovuka mipaka".



Mkuu wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Zainab Abdallah (kulia), akikabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Mkuu wa wilaya ya Pangani, Mussa Kilakala katika kijiji cha Masaka jana, kwa ajili ya kuanza kuukimbiza wilayani humo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Mafuriko yasababisha watu 1,000 kukosa makazi

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

WATU zaidi ya 1,000 hawana makazi mkoani Arusha kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha na kusababisha mafuriko ya maji kuingia katika makazi yao.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, alipotembelea maeneo yaliyoathirika jana, hasa eneo la Sakina, alibaini nyumba nyingi ziliharibika kwa kujaa tope.

"Tunaendelea kufanya tathimini zipo nyumba zaidi ya 1,000 zimeingia maji baada ya kukamilisha ndipo tutapata taarifa kamili," alisema Makonda.

Makonda, aliwataka wanachi kutafuta sehemu ya kujihifadhi na kuacha hali ya mvua ipite kwa kuwa tangu mwaka jana watabiri wa hali ya hewa walishaeleza kutakuwa na mvua za El-Nino.

"Wananchi wanaojijua wapo eneo ambalo siyo salama wanaweza kuondoka wasisubiri mpaka serikali iwatake wahame," alisema Makonda na kuongeza kuwa:

"Tujitahidi kuepuka haya mazingira hatuwezi kusema ondoka nenda sehemu fulani lakini wewe unauwezo wa kuona hapa nilipo si sehemu salama na sisi kama serikali tusingependa kutumia nguvu ya kuwaambia watu ondokeni hapa," alisema Makonda.

"Tumepata madhara makubwa na kubwa kuliko tumekata sana miti na tumejenga bila kufuata utaratibu, matokeo yake mazingira yanatuadhibu na wengine tuliambiwa hili eneo ni hatari lakini hawajataka kukubali matokeo yake ndio haya," alisema.

Aidha, Makonda alisema amepewa taarifa kuna utafiti ulifanyika wa kuona hali halisi nyakati za mvua nini kinafanyika na kifanyike nini kuokoa maisha ya wananchi, ripoti ilichukuliwa na kuwekwa kibindoni

"Katibu unayo hiyo ripoti mimi nimepatiwa jana hiyo ripoti na ilitumia fedha nyingi matokeo yake hiyo ripoti imewekwa kapuni," alisema Makonda.

Makonda alisema ataipitia ripoti hiyo na kuwatafuta wataalamu waliofanyia kazi ili ikiwezekana kurudi katika misingi ya awali kutibu tatizo hilo kwa lengo la jiji la Arusha kuwa la kitalii badala ya watu kushangaa wanaochukuliwa na mafuriko.

Aidha, Makonda alisisitiza suala la ujenzi unaozingatia mipango miji ili kuepuka athari zitokanazo na mafuriko na kuwataka madiwani kuwa na mipango ya muda mfupi na muda mrefu katika kunusuru kaya zilizoathirika na mafuriko.

## Rufaa kesi ya mbunge Gekul yatupwa

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MBUNGE wa Babati Mjini (CCM), Pauline Gekul, ameshinda kesi ya rufani ya udhalilishaji iliyofunguliwa na mfanyakazi wake, Hashim Ally katika Mahakama Kuu, Kanda ya Manyara, baada ya Jaji Devotha Kamuzola, kueleza ilani iliyotumika kufungulia kesi ya msingi haikukidhi vigezo vya kuitwa ilani.

Kutokana na mapungufu hayo ya kisheria, Jaji Kamuzola ametupilia mbali kesi hiyo namba 577 ya mwaka 2023, iliyokuwa ikimkabili mbunge huyo.

Katika kesi ya msingi, Gekul alikuwa akikabiliwa na shtaka moja la shambulio na kusababisha madhara kwa mwili, chini ya Kifungu cha 241 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16, Marekebisho ya Mwaka 2022.

Alikuwa anadaiwa yeye na watu wengine ambao hawako katika malalamiko hayo, Novemba 11 Mwaka 2023, Mjini Babati, mkoani Manyara, walimuita Hashim na kumuweka kizuizini.

Huku, wakimtishia kwa silaha ya moto, walimvua nguo na kumshambulia kwa kumlazimisha kukalia chupa ya soda ili iingie katika njia yake ya haja kubwa.

Wakati anasoma uamuzi huo, Jaji Kamuzola, alisema Mahakama hiyo inatupilia mbali shauri hilo kutokana na mapingamizi matatu yaliyotolewa na mjibu rufani, (Gelul) kumridhisha.


Nje ya Mahakama, Wakili Peter Madeleka, anayemwakilisha Hashim, alidai kuwa upande wa warufani, wameyapokea maamuzi ya Mahakama ila hawajaridhika nayo.

Madeleka alidai kuwa kati ya mapingamizi matatu ya Gekul, pingamizi moja lililotolewa limetosha kuiondoa kesi mahakamani.

Wakili Madeleka, amedai kuwa Jaji Kamuzola, amepotoka kisheria na alitafsiri vibaya kifungu cha 91 (1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA), na uamuzi wa Mahakama uliotolewa unaweza kukatiwa rufani, kwa kuwa unahitimisha kesi mahakamani.



Kutokana na uamuzi huo, Madeleka amedai kuwa wanakusudia kwenda Mahakama ya Rufani ya Tanzania na ikishindikana watakwenda Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (ACHPR) kufungulia kesi hiyo.



# Mume ajisalimisha polisi, adaiwa kumuua mkewe

**Na Rose Jacob,** MWANZA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mwanza linamshikilia Jackson Kalamji (49), mkazi wa Kijiji cha Mwamanyili Buchosa wilayani Sengerema kwa tuhuma za kumuua mkewe kwa kumchoma kisu kutokana na wivu wa mapenzi.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Wilbroad Mutafungwa alisema kuwa tukio hilo lilitokea Aprili 13 mwaka huu majira ya saa 7: 00 asubuhi nyumbani kwao baada ya mtuhumiwa huyo mkewe kuwa na uhusiano wa mapenzi na mwanaume mwingine.

" Ungomvi huo ulianza usiku, ilivyofika asubuhi Jackson alimuua Mariam kwa kumchoma choma na kisu sehemu mbalimbali za mwili," alisema.

Mutafungwa alisema kuwa baada ya mtuhumiwa huyo kufanya mauaji hayo, alikimbia lakini kila eneo alilokuwa akitokea alikuta watu wakimtafuta, kitendo ambachoi kililmlazimu kujisalimisha Kituo cha Polisi Buchosa.

Alisema uchunguzi ukikamilika mwili wa marehemu utakabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya maziko na kwamba kwa sasa umehifadhiwa Hospitali ya Wilaya ya Sengerema.

Katika tukio jingine; Jeshi hilo linawashikilia Augustine Brayson (40), Mkazi wa Mecco wilayani Ilemela na Fatina Abdul (40), Mkazi wa Nyashishi Misungwi kwa tuhuma za kukutwa na magunia 16 ya dawa za kulevya aina ya mirungi.

"Watuhumiwa hawa walikutwa wameficha mirungi katika vichaka maeneo ya Fela Usagara wilayani Misungwi, tunawashukuru wananchi kwa kutoa taarifa na polisi tulifuatilia na kuwakamata," alisema Kamanda Mutafungwa.

Alisema watuhumiwa hao watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.



Mbunge wa Musoma Vijijini, mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo akizungumza na baadhi ya walimu na viongozi wa Kata ya Bulinga jana, alipokwenda kukabidhi mifuko 100 ya saruji, kwa ajili ya uboreshaji wa miundombinu ya Shule ya Sekondari Bulinga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali watoboa siri kukosa nembo ya TBS

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

UTENGENEZAJI wa bidhaa zisizokuwa na ubora unaohitaji katika soko la ndani na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) unasababisha wajasiriamali wengi nchini kukosa nembo ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS), imeelezwa.

Hayo yalielezwa jana na wajasiriamali wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga katika mafunzo ya uzalishaji, usindikaji na ufungashaji wa bidhaa za uokaji yaliyotolewa na TBS Kanda ya Ziwa.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Shamu Saidi alisema kuwa utengenezaji wa bidhaa zisizo kuwa na ubora ni chanzo cha kuendelea kukosa nembo ya TBS na kubaki na soko la ndani ambalo ushindani wake ni mkubwa.

Shamu aliiomba TBS kuendelea kuwapatia elimu endelevu ya namna sahihi ya utengenezaji na ufushangashaji wa bidhaa wanazozalisha na kupata nembo ya shirika hilo baada ya kukaguliwa na wataalamu wa shirika hilo.

" Bidhaa nyingi tunazalisha majumbani mwetu hasa mikate na zile za usindikaji ambako mazingira yake sio rafiki kwani kuna mwingiliano mkubwa wa wanafamilia na majirani ndiyo sababu tunapozipeleka ofisi za TBS kuangalia viwango na kupata nembo, lakini zinakutwa hazina sifa na kutupwa," alisema.

Aaliiomba Ofisi ya Mkuu wa Wilaya iwapatie maeneo ya wazi pembezoni mwa barabara kwa kuwa yana mandhari nzuei ya maua na miti ili wajenge viwanda vidogo vya kuoka mikate na kusindika bidhaa hali ambayo itasaidia kutangaza bidhaa na kupata masoko ya uhakika.

Abdullah Juma, alisema elimu watakayoipata itawawezesha kujenga imani kwa wateja wao bidhaa wanazozalisha ni salama kwa matumizi ya binadamu kwa kuwa zitakuwa na nembo ya ubora ya TBS.

Meneja wa Mafunzo na Utafiti wa TBS wa kanda hiyo, Hamisi Sudi alisema kuwa wafanyabiashara na wajasariamali wanazalisha bidhaa nyingi ambazo hazina viwango na ubora unaohitajika na kushindwa kukabiliana na ushindani katika soko la ndani na EAC.

Sudi, alisema elimu wanayotarajia kuitoa kwa wajasirimali hao ni pamoja kufahamu mahitaji ya soko la EAC, viwango vya ubora wa bidhaa wanazozalisha na faida.

Alitaja nyingine ni kupata elimu ya matakwa ya viwango vya bidhaa za uokaji, usajili wa biashara, kanuni bora za usindikaji na utaratibu wa uthibitisho wa ubora wa bidhaa.

Akifungua mafunzo hayo, Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita alitaka TBS kuongeza wigo wa kuwafikia na kuwaelimisha wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo ili kuwa na bidhaa bora ambazo zitalinda afya mtumiaji wa mwisho na kukabiliana na ushindani katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

## 'Wananchi lipeni kodi, tozo ili kurahisisha upatikanaji maendeleo'

**Na Neema Sawaka,** MSALALA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, Khamis Katimba amewataka wananchi kulipa tozo na kodi katika halmashauri hiyo ili kurahisisha upatikanaji maendeleo kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

Katimba alitoa wito huo wakati wa uzinduzi wa stendi mpya ya mabasi ya Isaka.

Alisema serikali inajitahidi kutekeleza malengo yake kama ilivyoahidi, hivyo wananchi nao wajitahidi kulipa tozo na kodi.

"Serikali ni ya wananchi, tunapaswa kulipa tozo za serikali na kujiepusha na utoroshaji au ukwepaji wa kulipa kodi kwa kuwa fedha zinazokusanywa hutumika kwa shughuli za maendeleo ya jamii ikiwemo ujenzi huu wa stendi," alisema Katimba.

Alisema stendi hiyo ni moja ya mipango ya muda mrefu ya serikali na uzinduzi wake utaleta nafuu na kuongeza wigo wa kukuza uchumi wake na wa wananchi.

Alitoa wito kwa wananchi kuitumia ipasavyo stendi hiyo kwani uwepo wake ni moja ya sababu za ukuaji wa mji wa Isaka.

"Changamkieni viwanja kwani halmashauri imevipima karibu na stendi pembezoni mwa Barabara ya Isaka-Rwanda, pia stendi hii imelenga kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji itachangia halmashauri yetu kuongeza mapato kwa ajili ya kuhudumia wananchi kwani ni chanzo cha uhakika, " alisema.

Alisema na timu yake ya wataalamu, wataendelea kuhakikisha mapato yanakusanywa na kutumika kama inavyoelekezwa na serikali.

Alisema hadi kufika Machi 31, mwaka huu, halmashauri hiyo imekusanya asilimia 91 ya makusanyo ya Mfuko Mkuu ambayo ni sawa na Shilingi bilioni 4.6.

Ofisa Mapato wa Halmashauri hiyo, Salehe Msosole, alishukuru uongozi wa halmashauri kwa kuweka msisitizo utendaji kazi uliotukuka kwa watumishi wake na kusaidia kuongeza mapato.

"Ukweli ulio wazi ni kuwa, ushirikiano wa Mwenyekiti wa Halmashauri, Mibako Mabubu na mkurugenzi wetu (Katimba) pamoja na watumishi umesaidia sana halmashauri hii hasa kuweka kipaumbele cha kwanza katika utendaji kazi wa kila siku," alisema na kuongeza kuwa:

"Hiyo imesababisha usimamizi mzuri wa mapato hasa msisitizo wa kila diwani katika eneo lake huhakikisha tozo za serikali zinalipwa kama inavyotakiwa."

Alisema Mkurugenzi huyo aliunda kikosi kazi kufanya doria usiku na mchana kuhakikisha wanadhibiti utoroshaji wa mapato.

"Tangu waanze usimamizi huu kila siku wanakamata magari yasiyopungua manne na Bajaj mbili," alisema na kutoa wito kwa wafanyabiashara kulipa tozo za halmashauri kwa hiyari ili kujenga uchumi wa nchi na kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan .

Diwani wa Kata ya Isaka, Majuto Pazi, aliwaomba wananchi kutumia fursa hiyo kujiongezea kipato.

"Namshukuru Rais Samia kwa kuleta fedha za kuwezesha kujenga stendi hii sanjari na Mbunge wa Jimbo la Msalala, Idd Kassim Idd kwa ushawishi, kusimamia na kuhakikisha serikali na wawekezaji wanatoa fedha kwa wakati ili kutekeleza miradi ndani ya halmashauri," alisema.



Ukurasa 12

**Ilivyo DRC yenye maafa, wakimbizi, shule na jimboni Kivu zimefungwa**





Ukurasa 14

**Zuma; babu mwenye miaka 81 anayejihisi ana nguvu kuongoza**

siasa

JUMATANO APRILI 17, 2024

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU

# Siasa za Samia zinavyovuka na mitaji ya historia awamu tano zilizotangulia

**Na Peter Orwa**

MARA alipoingia madarakani, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan miaka mitatu na miezi kadhaa sasa akaja na kaulimbiu 'Kazi Iendelee. 'Awali akiwa mkuu wa pili wa nchi, alikuwa sehemu ya kaulimbiu 'hapa kazi tu.'

Je linapokuja swali la kumtafsiri kisiasa, Rais Dk. Samia, anayetumikia awamu ya sita sasa, anasimama wapi, jibu linaangukia tafsiri mtambuka.

Mosi, ni mtaalamu wa Utawala, pia Uchumi wa Maendeleo. Daima, safari yake yote, hajawahi kuwa nje ya maeneo hayo, ingawa ninamuongezea taaluma ya matendo na falsafa zake tatu.

Mara zote yu muumini wa fani Mazingira, eneo alilodumu nalo sana katika utedaji serikalini, vilevile akibaki kuwa Mama wa kwanza kushika usukani wa kuongoza nchi, daima hajakaa mbali, anadumu kwa matendo katika haki za kijinsia na vijana.

Kimsingi, Dk. Samia anatumikia Awamu ya Sita sasa, ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kinachoendelea kushika nafasi, hivyo itikadi, sera na ilani zake zina mfumo wa kudumisha ya CCM.


Je kisiasa yu wa namna gani? Dk. Samia ni muumini wa kuendeleza ya chama chake - CCM, hali kadhalika 'kazi inaendelea'. Hapo katika Awamu ya Tano alikuwa sehemu ya kubuni na kuyasimamia.

Mbali na mradi mkubwa, reli ya SGR na Bwawa la Umeme Mwalimu Nyerere, ilianza kutekelezwa katika Awamu ya Tano, safari zake ni za mbali.

Bwawa la Mwalimu Nyerere likiwa na chimbuko la Awamu ya Kwanza, huku SGR dodoso zake zikaanza katika Awamu ya Pili, kwa Rais Jakaya Kikwete zote sasa ni 'bidhaa' za Awamu ya Sita.

Ni katika eneo hilo, Rais Dk. Samia, anaonekana kuwa na chembe za Rais Mzee Ali Hassan Mwinyi, pia za Rais Kikwete.

Staili yake ya uongozi kisiasa amekuwa akitumia zaidi mfumo wa maridhiano na kuelewana kisiasa, na hiyo ikaonekana mapema tu baada ya kuingia madarakani Januari mwaka 2021, akatamka kuja na falsafa hiyo ya maridhiano.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokutana na Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA, Tundu Lisssu. **PICHA: MTANDAO**

Hizo akazitaja kwa Kiingereza; 'reconciliation, resilience, reforms na rebuilding', akimaanisha 'upatanishi, ustahimilivu, mabadiliko na ujenzi upya'.

Hayo muda mfupi baadaye akaonekana kuanza kuzitelekeza katika matukio mbalimbali kama vile kufungulia mjumuiko wa kisiasa uliokuwa umezuiwa na kuachiwa washitakiwa wa kisiasa.

Vilevile, kuna mjumuiko katika ulingo wa siasa kwa vyama hasimu, kama vile kuwa anapokuwa mgeni rasmi katika Mkutano Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa CHADEMA.

Hadi sasa Rais, Dk Samia, pia ni Mwenyekiti wa CCM, amekuwa mstari wa mbele kuwaunga mkono vyama vya upinzani katika kulisukuma dai lao kuu la kuandikwa Katiba Mpya.

Ni mtazamo ukaonyeshwa kwa kiasi kikubwa na Rais Ali Hassan Mwinyi, Mwenyekiti wa CCM, aliyeukaribisha mfumo huria kiuchumi mwaka 1985 na mwaka 1992, akawezesha mabadiliko kisiasa.

Kisheria, nchi ikaingia katika siasa ya vyama vingi; ikibeba sura kuu ya maridhiano ya utashi tofauti wa kisiasa nchini na hata kukashuhudiwa uchaguzi wake mwaka 1995 tangu ifungwe kisheria mwaka 1964.

Tena, Dk. Samia anashabihiana katika dhana maridhiano na Rais Kikwete, akifungua mlango wa mjadala wa Katiba Mpya, hata akaliundia bunge maalum, ingawaje halikufika mbali.

Samia ndiye aliongoza Bunge la Katiba, kikao kilichompa sifa na heshima anayodumu nayo hadi sasa, kutokana na umahiri na busara zake kazini, akiwa mezani pale kikaoni Dodoma.

Sambamba na hayo, kama inavyojulikana uongozi wa siasa unavyohitaji ustahimilivu, mifano ya yaliyofanywa na Mzee Mwinyi na kijana wake Kikwete, unasaba wake uko wazi sasa katika nyendo zake Rais Dk. Samia.

INAENDELEA UK. 14

# Ilivyo DRC yenye maafa, wakimbizi, shule za jimboni Kivu zimefungwa



Askari wa Tanzania walioubeba mwili wa mwenzao, aliyeuawa nchini DRC, karibuni. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

SIMULIZI si nzuri maana ilikofika, askari wa Kitanzania watatu waliokuwa sehemu ya vikosi vya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), nchini Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), pia mwenzao mmoja wa Afrika Kusini wameuawa.

Leo hilo lina wiki moja, ikiakisi uhalisia wa hali mbaya iliyoko DRC, hata katika jimbo la Kivu penye mapigano kati ya vikosi serikali na waasi nchini humo. Mapigano yasiyoisha miongo kadhaa, mashambulizi hasa kutoka waasi wa M23.

Tangu mwezi Desemba mwaka jana, SADC imepeleka kikosi mkoani Kivu Kaskazini, kinachoundwa na wanajeshi kutoka; Afrika Kusini, Tanzania na Malawi kusaidia vikosi vya serikali ya DRC kupambana na waasi hao wa M23, inayodaiwa kusaidiwa na Rwanda, huku yenyewe ikikanusha vikali.

Ni suala tata kwani kabla ya vikosi hivyo vya SADC, pia wakawapo wenzao waliofika kwa madhumuni hayo, kisha wakaondoka kutokana na madai ya kiwango cha uwajibikaji wao.

Mwanzo, SADC ikatangaza kuuawa askari wake, mnamo Februari 15 wakati wanajeshi wawili wa Afrika Kusini walipouawa kwa bomu karibu na Goma, mji mkuu wa mkoa wa Kivu Kaskazini.

Hayo yanaendelea, huku kwa wenyeji hali ni mbaya, kundi kubwa la wakimbizi na matokeo ya vifo, hata sikukuu za Pasaka na Iddi Elfitri zilizopita hivi karibuni, wenyeji walinukuliwa kuona kama haiwahusu, wako katika shida.

> Kupitia vita watoto kwa leo hawako tena ndani ya masomo. Masomo (shule) imebaki ni 'ma- camps' (kambi) ya majeshi na watoto leo wanazunguka mitaani, sababu ya vita hawana walimu!...

**SHULE 'ZABUMA'**

Kuna vilio tangu mwezi uliopita, kwamba hali ya wakimbizi wa vita vya M23, wanaokwepa hali mbaya. Sasa imeathiri mno ustawi wa elimu katika mji wa Goma, baadhi ya shule zinashindwa kuendesha masomo kwa sababu ya ugeni wa wakimbizi katika majengo yao.

Wanafunzi wanaomimika Goma, wanakimbia mashambulizi ya vikosi vya DRC na waasi wa M23, wakizuia masomo kuendelea.

Wakimbizi hao walioingia katika mji wa Goma, wengi sasa wamejazana kwenye madarasa ya shule, hali iliyotajwa mwezi uliopita kuzuia kalenda za masomo.

Mmiliki wa Shule ya Msingi Lac Vert, Hangi Bahati, akabainisha kuwa tangu wakati huo, watoto wamekuwa mitaani, akiwa na ufafanuzi:

"Kupitia vita watoto kwa leo hawako tena ndani ya masomo. Masomo (shule) imebaki ni 'macamps' (kambi) ya majeshi na watoto leo wanazunguka mitaani, sababu ya vita hawana walimu!..."

Mamlaka ya elimu ya msingi mkoa wa Kivu Kaskazini, inasema elimu imeathirika kitaifa, Ofisa Mkuu wa Elimu Kaskazini mwa Kivu, Luc Baweza Kabango, naye anaelezea:

"Tangu vita vilipoanza zaidi ya miaka miwili iliyopita, utaona kwamba mambo yanabadiliki, yaani shule nyingi zimefungwa na kuna watoto ambao hawasomi.

"Itabidi tufanye kazi kubwa kwa sababu akili za watoto zinaathiriwa na migogoro ya silaha, kuna watoto wengine ambao pia watakuwa kama wanyama au waasi. Hii inaharibu vipengele vyote vya elimu," analalamika.

Mjini Goma, wapiganaji wa M23 wanaendeleza mashambulizi kwenye maeneo ya; vijiji vya Katanda na Mayi ya Moto, vilivyoko kilomita chache kutoka Vitshumbi sasa wanapadhibiti.

Wiki tatu ziliyopita, serikali imewataka wakimbizi waliokimbilia kujisitri shuleni waondoke, kuruhusu watoto kurejea shuleni masomo yaendelee.

Hata hivyo, wazazi wa wazazi wa watoto bado wanakabaki na wasiwasi ya hali hiyo, hata kuwazuia watoto kubaki nyumbani wasiende shule, hadi watakapohalikisha mustakabali mzuri wa kiusalama.

Bora Batende, ni mzazi wa mwanafunzi mmoja na ambae anayesema kabla ya vita, wanawe ilikuwa wanasoma na kutokana na hali hiyo amewazuia.

Watu waliokimbia vita, pia nao wanaishi shuleni kwenye madarasa wakisema wanapenda kuondoka katika makazi hayo shuleni, ila hawana mbadala pa kwenda, pia hata hawana vifaa vya kujenga mahema ya muda katika kambi walizoelekezwa.

Mkimbizi Bibiche Ndoole, ana maelezo yake kwamba:"Tulikimbia vita ya M23, tuliona mashambulizi yanakuwa mengi, ndugu zetu wengi wameuawa, ndio sababu tukakimbia na kuja kujihifadhi hapa shuleni.

"Kwa sasa tunashindwa kujua mahala pa kwenda, tunafahamu wanafunzi wa hapa Mugunga hawawezi kusoma kwa sababu yetu."

**MACHUNGU HALISI**

Shirika la Umoja wa Mataifa la Wakimbizi (UNHCR), tayari mwezi uliopita likataja watu milioni 5.7 wamelazimika kuwa wakimbizi ndani Mashariki mwa DRC.

Aidha, kupitia taarifa iliyotolewa na msemaji wa shirika hilo, Mathew Saltmarsh jijini Geneva Uswisi, ni kwamba imeshatoa wito wa kuchukuliwa hatua za haraka kutokana na ongezeko la hatari kwa watu waliokimbia makazi yao Mashariki mwa DRC,

Hiyo inapokewa na kauli ya baba wa watoto sita, anayetafuta usalama kwa familia yake katika eneo la makazi ya muda karibu na Goma, baada ya mkewe kuuawa na bomu huko Sake, jimbo la Kivu Kaskazini.

"Miaka miwili ya mizozo katika maeneo ya Kivu Kaskazini huko Rutshuru na Masisi, imewalazimu zaidi ya watu milioni 1.3 kukimbia makazi yao ndani ya DRCna kusababisha jumla ya watu milioni 5.7 kuwa wakimbizi wa ndani katika majimbo ya Kivu Kaskazini, Kivu Kusini na Ituri," inaeleza UNHCR.

Msemaji huyo anaongeza kuwa, tangu mapigano makali yashike kasi katika mji wa Sake, tarehe 7 Februari, karibu watu 300,000 wamewasili katika jiji la Goma, ambako hali ilikuwa mbaya.

Watu zaidi ya 85,000 walikuwa wamekimbia ghasia hizo hizo na kutafuta makazi katika eneo la Minova la Kivu Kusini, ambalo tayari lilikuwa limepokea watu 156,000 waliokimbia makazi yao tangu Januari mwaka huu.

Kwa mujibu wa UNHCR, kuna shambulio la makombora katika kituo cha biashara lililofanyika Machi 20, hata likamuua mwanamke mkimbizi wa ndani na kuwajeruhi wengine watatu, wakiwaemo watoto wawili.

Ripoti za milipuko ya mabomu ya kiholela huko Sake na Goma katika wiki za hivi karibuni, imeshaua zaidi ya watu 30 na kujeruhi takriban 80, hadi wiki tatu zilizopota.

Mwaka jana kuna shule 25 zilichukuliwa na vikundi vyenye silaha visivyo vya serikali katika maeneo ya Masisi na Rutshuru pekee, na zingine 17 zilishambuliwa. Mwaka huu, pia shule saba zimeharibiwa na milipuko ya mabomu.

Pia mwaka jana katika eneo la Kivu Kaskazini pekee, UNHCR inaripoti mikasa 50,159 zilizoripotiwa za unyanyasaji kijinsia, zaidi ya nusu ya nusu ni ubakaji, ndai yake asilimia 90 ya waathirika walikuwa wanawake na wasichana, wakati asilimia 37 ni watoto.

Hilo linaifanya UNHCR kukemea kukomeshwa moja kwa ghasia hizo, ikizitaka pande zote katika mzozo kuheshimu na kuzingatia sheria za kimataifa za kibinadamu, kwa kuwalinda raia.

Pia, inataja hifadhi ya kibinadamu ziliongezeka katika majimbo ya Mashariki, ikitolewa takwimu kati ya Juni na Desemba mwaka jana, msaada wa kuokoa maisha ulifikia zaidi ya watu milioni 3.1.

UNHCR imetoa hifadhi ya

INAENDELEA UK. 13

# Ilivyo DRC yenye maafa, wakimbizi, shule za jimboni Kivu zimefungwa



Ndivyo yalivyo madhila wanayopata wakimbizi wa vita, huko Goma, DRC. **PICHA: MTANDAO**

**INATOKA UK. 12**

dharura kwa zaidi ya watu 40,000 walio katika mazingira magumu waliofika Goma.

### ILIKOTOKA DRC

Kijiografia, ina mji mkuu Kinshasa. Ni nchi ya pili kwa ukubwa barani Afrika na 11 duniani, wakazi wake wanakadiriwa milioni 12, umaarufu wao duniani, magwiji wa muziki wa dansi.

Hata hivyo, tangu kupata uhuru mwaka 1960, hawajawahi kufadi utulivu na amani ya kudumu. Majirani wao ni mataifa; Jamhuri ya Afrika ya Kati, Zambia, Rwanda, Burundi, Angola na Tanzania kupitia Ziwa Tanganyika.

Wakati inapata uhuru iliitwa taifa la Congo, ikiongozwa na Waziri Mkuu, Patrice Lumumba. Hakudumu, aliuawa katika mapinduzi, nafasi yake ikachukuliwa na Mobutu Sese Seko Wazabanga Kuku, mwaka 1965.

Mwaka 1971, Rais Mobutu akabadili jina la nchi kuwa Zaire, akiendelea na utawala uliotajwa wa kidikteta hadi mwaka 1997, alipong'olewa na wana -mapinduzi waliojipanga nje ya mipaka, wakampa urais, mpambanaji mwenzao na mkazi wa Dar es Salaam, Laurent Desire Kabila.

Hapo naye akabadili jina la nchi kuwa DRC, akidumu madarakani hadi mwaka 2001 alipouawa na mmoja wa walinzi wake.

Ni hali iliyochangia machafuko mengi ndani ya nchi, kukiwapo makadirio kati ya mwaka 1998 na 2003 kumesababisha vifo vya watu milioni 5.4.

Ni wakati ulioshuhudiwa vikundi vingi vya waasi, vikileta machafuko makubwa ya kisiasa, badhi ya waliomuunga mkono Marehemu Mzee Kabila, Profesa Wamba Dia -Wamba, ambaye akamuasi na kujiunga na kikundi cha uasi Rally for The Congolese Democracy (RCD), ambacho kikapatwa na msuguano wa ndani kuzaa, RCD - Goma na RCD -Kisangani, iliyoongozwa na Wamba.

Pia, kukawapo kikundi kingine kilichosumbua DRC kupigana nayo chini ya muasi, Dk. Bizimana Karahamuheto au umarufu wake Bizima Karaha, anayedaiwa na unasaba wa uraia jirani, alianza uasi mwaka 1998 dhidi ya Rais Laurernt Kabila, baadaye aliposhindwa akakimbilia nchini Afrika Kusini.

Taifa likiwekwa chini ya mwana wa Laurent Kabila, aitwaye Joseph, mwanafunzi wa Shule ya Sekondari ya jioni Zanaki (iliyokuwapo wakati huo) jijini Dar es Salaam na Sangu ya Mbeya kwa kidato cha tano na sita, akaongoza nchi kuanzia mwaka 2001 hadi 2019.

Ni zama zinazotajwa, akafanikishaa kutimiza hali ya hewa ya vita na hata akaondoka madarakani, kwa kuwezesha kuwapo uchaguzi wa amani wa kwanza DRC, mwaka 2018 tangu uhuru wake akimuachia madaraka.

Hata hivyo, ukanda wa Mashariki ya Congo, ambako kunazugumzwa Kiswahili, kumebaki na historia ya chokochoko ikishuhudiwa zaidi tena kuanzia mwaka 2015, hali inayoendelea hadi sasa.

Vita hivyo, vyanzo vya vita visivyoisha vitanja kuzaliwa na mambo mawili: Moja, ni lile o Rais Tshishekedi, aliye madarakani kwa awamu ya pili, baada ya kushinda uchaguzi karibuni, anaishutmu majirani – Rwanda.

Liingine ambalo ndilo kuu, unatajwa utajiri wa madini na hasa shaba, mataifa ya kigeni na matajiri yakielezwa wana mkono kama ngazi ya kufikia rasilimali hiyo.

Ni utajiri unaopatikana katika majiji yake makubwa kama Kinshasa, unaoufutiwa na Lumubashi,a wa tatu, Mbuji Mayi.

Raia wake wamekuwa wakitapatapa, huku Umoja wa Mataifa katika Ripoti ya Maendeleo ya Binadamu, inaitaja DRC kushika nafasi ya 179 kati ya 191 kimaendeleo. Kuna raia 600,000 wanaotajwa kuishi nchi jirani na watu milioni 4.5 wamehama makazi yao.

## Siasa za Samia zinavyovuka na mitaji ya historia awamu tano

**INATOKA UK. 11**

### NGOME YA MAENDELEO

Katika safari ya maendeleo, anaonekana kubebwa kwa 'kazi iendelee', yake mambo yaliyoasisiwa na Mwalimu Nyerere katika Mpango wa Maendeleo ya Nchi ya Kwanza wa mwaka 1964 hadi 1969.

Hizo ni kuwatosheleza Watazania hasa katika mahitaji ya Elimu, Kilimo na Afya na marais wa awamu zote zilizomtangulia, hawajawahi kuziacha.

Mathalan, mikakati ya kilimo nchini ambayo Rais Nyerere, pia elimu ya msingi, Rais Mkapa akaelekeza nguvu katika kuboresha na kutanua wigo, Rais Samia sasa amezama katika kuongeza mtaji wa kibajeti na kilimo cha kisasa.

Ndio picha inayofanya kilimo cha Kitanzania kikiwekezwa bajeti maradufu kutanua umwagiliaji, soko la mazao kama ya ufuta, miradi maalum ya kuingiza vijana katika ajira ya kilimo cha kisasa, huku mbolea ikikuzwa maradufu kwa viwanda nchini ikiwa na wakala mpya.

Rais Dk. Samia mwenyewe amekuwa akinadi kilimo nchini nje ya mipaka kuanzia soko, hadi ukaribishaji mitaji, ili kuleta mapinduzi kilimo alichotetea Mwalimu Nyerere kwa dhana "kilimo ndio uti wa mgongo wa taifa.'

Hiyo ndiyo inayoangaliwa katika maboresho ya Sekta ya Elimu, kuanzia mfano Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) na kama huo wa sekondari uitwao MMES, katika Awamu ya Tatu, Rais Kikwete akabuni Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM), vyote sasa Rais Samia anaviendeleza, kama miradi mikubwa kitaifa.

Ushahidi wake uko katika idadi zaidi ya zahanati na vituo vya afya 300 kuona zinafikisha huduma katika kata, vilevile sera hiyo katika shule, MMEM na MMES ikiboreshwa, sasa shule maalum za wasichana na utatuzi wa kero na mahitaji shuleni zikibeba ajenda kubwa.

Kiuchumi, wakati Mzee Mwinyi akaonyesha wazi kuwa muumini mkubwa wa ushirikishaji sekta binafsi, mrithi wake Rais Mkapa, akaunda Tume ya Rais ya Kubinafsisha Mashirika ya Umma (PSRC). Kinachofanyuwa sasa katika Awamu ya Sita, ni kuzipa nafasi sekta binafsi, inayoakisi matendo hayo ya wakuu wa Awamu ya Pili na Tatu.

Hiyo inamfanya Rais Dk Samia, kuwa madarakani leo ana sura zote zilizotangulia na falsafa ya kubeba chama chake, ikithibitisha kaulimbiu 'kazi iendelee' na ndio maana miradi mikubwa kitaifa imo Bwawa la Mwalimu Nyerere na SGR, ya Awamu ya Tano.

Pia, inaungana na 'Elimu Bure' ambayo imeboreshwa maradufu katika awamu yake, kuwezesha Watoto wa Kitanzania kunufaika na elimu yao, kuanzia ngazi ya shule hadi vyuo, mtaji wao sasa ni juhudi zao kuelekea kufaulu masomo.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Zuma; babu mwenye miaka 81 anayejihisi ana nguvu kuongoza

• Alifungwa, sasa ameshinda mahakama yampa ruksa



Mzee Jacob Zuma, katika picha tofauti, **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

NCHI ya Afrika Kusini, ambayo inaongozwa na chama tawala cha African National Congress (ANC), inatarajia kufanya uchaguzi mkuu Mei 29 mwaka huu.

Katika uchaguzi huo, mwanasiasa mkongwe ambaye pia amewahi kuwa Rais wa nchi hiyo, Jacob Zuma kabla hajafukuzwa ANC, anatarajia kuwania urais kupitia chama chake kipya cha uMkhonto we Sizwe (MK).

Zuma anaingia katika kinyang'anyiro baada ya Mahakama ya Uchaguzi nchini humo, kubatilisha uamuzi uliomwekea kikwazo kiongozi huyo kugombea urais katika uchaguzi huo.

Awali, Tume Huru ya Uchaguzi nchini humo ilimtengua Zuma kutogombea nafasi hiyo kwa mara nyingine kutokana na rekodi za uhalifu alizokuwa nazo.

Hata hivyo, baada ya mahakama kumpa kumruhusu, ni wazi sasa atachuana na Rais wa sasa Cyril Ramaphosa aliyetangazaza siku ya Jumatano kuwa uchaguzi mkuu wa nchi hiyo utafanyika Mei 29.

Tume ya Uchaguzi, nayo imetamka itakata rufani kusimamia uamuzi wake Zuma, asigombee.

Chama ambacho kitashinda wingi wa viti katika bunge lenye viti 400, vitamchagua Rais. Ramaphosa anagombea muhula wa pili wa miaka mitano ya mwisho.

Zuma mwenye umri wa miaka 81, atagombea nafasi hiyo kupitia chama chake kipya alichokisajili baada ya kujitoa uanachama wa chama chake cha zamani cha ANC ili kuendelea na harakati za kisiasa.

> Zuma mwenyewe amekuwa akipiga kampeni kwa niaba ya chama cha upinzani cha uMkonto we Sizwe (MK) kwa lengo kufufua tena hadhi yake, akidai kuwa wanachama wa ANC ni wasaliti.

### KUONDOLEWA ANC

Mwaka 2018, Zuma alijiuzulu nafasi ya urais baada ya shinikizo kutoka katika chama chake cha zamani cha ANC, ingawa alipimga sana uamuzi wa kumshikiniza kujiuzulu.



Kiongozi huyo aliyeingia madarakani tangu mwaka 2009, alikuwa akikumbwa na shutuma nyingi za ufisadi. Pamoja na kujiuzulu ameendelea kuandamwa na wabaya wake kisiasa.

Katika kesi yake kuna shahidi mmoja aliyewahi kumshtumu kuwa alikuwa akipokea rushwa kila mwezi kutoka kampuni ya usalama, katika kashfa nyingine, ikaelezwa kuwa alilipwa fedha taslimu, zilizowekwa kwenye mkoba na kupelekwa na mtu maalumu.

Hiyo inatokana na kwamba, bado hawajaridhika na hukumu iliompa ruhusa ya kuwani urais, na huenda wanamhofia, kwani wachambuzi wa siasa za kimataifa wanasema chama chake kipya hakitabiriki katika kinyang'anyiro hicho, kwamba kinaweza kupenya.

Hayo ni kwa sababu wanaeleza kuwa kina ushawishi mkubwa katika jimbo analotoka Zuma la KwaZulu-Natal, huku akiahidi kubadilisha Afrika Kusini na inasemekana kuwa chama tawala kiko katika hatari ya kupata chini ya asilimia 50 ya kura kwa mara ya kwanza tangu kilipoingia madarakani mwishoni mwa enzi ya utawala wa ubaguzi.

Zuma mwenyewe amekuwa akipiga kampeni kwa niaba ya chama cha upinzani cha uMkonto we Sizwe (MK) kwa lengo kufufua tena hadhi yake, akidai kuwa wanachama wa ANC ni wasaliti.

Aidha, mwanasiasa machachari nchini humo, Julius Malema na chama chake cha Economic Freedom Fighters (EFF) naye ni miongoni mwa walioshiriki katika harakati za kuhakikisha Zuma anatoka madarakani.

### JACOB ZUMA NI NANI?

Historia inaonyesha kuwa yeye ni miongoni mwa wapigania uhuru wa Afrika Kusini na kwamba, akiwa na miaka 17, alijiunga na ANC na kuwa mwanachama hodari katika tawi lake la jeshini Umkhonto We Sizwe, 1962.

Katika harakati hizo za kutafuta uhuru wa nchi hiyo, alihukumiwa kwa kula njama za kutaka kupindua serikali ya kibaguzi na kufungwa miaka 10 katika gereza la watu hatari zaidi katika kisiwa cha Robben pamoja na Nelson Mandela.

Inaelezwa kuwa Zuma alikuwa akichochea morali ya wapigania uhuru kwa nyimbo na tungo za kizalendo na wengi wanaamini kuwa hicho ndicho kilimfanya kuwa maarufu miongo ni mwa wananchi wa vijijini kabla ya kuupata urais.

Yeye ni miongoni mwa waliioishi Morogoro Tanzania wakati wa kupigania uhuru wa nchi yao, baadaye alikuja kuwa Rais wa Afrika Kusini kabla ya kujiuzulu kwa kashfa.

Hata hivyo, akiwa madarakani, mwanasiasa machachari nchini, Julius Malema na chama chake cha Economic Freedom Fighters (EFF) walifanya mara kadhaa majaribio kutaka kumtoa madarakani.

Mwisho wake mwaka 2018 Zuma aliondolewa madarakani, hata hivyo, katika hatua hizo za kumzima kisiasa, mwanasiasa huyo mkongwe akaibuka na chama chake kipya.

Zuma ndiye aliyemrithi Thabo Mbeki ambaye naye alijiuzulu nafasi hiyo mwaka 2008 na kuamua kujiweka pembeni. Lakini kwa Zuma sivyo, bado anaendeleza harakati za kisiasa kupitia chama chake.

Mbeki aliiongoza Afrika Kusini tangu Nelson Mandela alipostaafu mwaka 1999 na alikuwa akitarajiwa kung'atuka mwaka 2009 lakini akajiuzulu na kumpisha Zuma ambaye naye yalimkuta mwaka 2018.

Hata hivyo, pamoja na kumwekea zengwe akajiuzulu, Zuma bado hajapoa, wachambuzi wa siasa za kimataifa wanasema, huenda akafanya maajabu katika uchaguzi ujao, licha ya umri kumtupa mkono.





## Ulega ataja mafanikio miaka 60 ya muungano mifugo, uvuvi

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ametaja mafanikio yaliyopatikana katika miaka 60 ya muungano mojawapo ni kuandaa mradi mkubwa wa miaka mitano utakaogharimu Dola za Marekani milioni 117, unaolenga kuleta mageuzi kwenye sekta ya uvuvi na ufugaji samaki.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu ushirikiano wa Tanzania Bara na Zanzibar kwa miaka 60 katika sekta ya mifugo na uvuvi, Ulega alisema fedha hizo ni mkopo na utekelezaji wake utaanza kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Alibainisha kuwa mradi huo umeandaliwa kwa pamoja kwa kushirikiana na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar.

Alifafanua kati ya fedha hizo kiasi kitakachotumika kwa Tanzania Bara ni Dola za Marekani milioni 65, Zanzibar ni Dola za Marekani milioni 41 na Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu itapatiwa Dola za Marekani milioni 10.

Kuhusu mwani, Waziri Ulega alisema serikali imeendelea kuimarisha zao hilo katika pande zote za Muungano ambapo kwa mwaka wa fedha uliopita zaidi ya Sh.milioni 400 zimetolewa kwa ajili ya kuongeza chachu ya kilimo hicho kwa wanawake.

Alisema hadi sasa tani 5,000 zinazalishwa Tanzania Bara na wataalamu wameanza kufanya utafiti ili mwani utumike kutengeneza bidhaa za chakula cha mifugo kutokana na kuwa na virutubisho vya kutosha.

Kuhusu sekta ya mifugo, Ulega alisema kwa kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan kutokana na kuimarisha diplomasia, nyama tani 35,297 zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 146.43 zimeuzwa nje ya nchi.

# Bil.500/- zahitajika kukarabati barabara, madaraja yaliyoathiriwa na mvua nchini

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa ameeleza kuwa tathmini ya athari ya miundombinu ya barabara nchini imebaini hadi kufikia Aprili 14, 2024 Sh.bilioni 500 zinahitajika ili kuwezesha urejeshaji miundombinu ya barabara na madaraja yaliyoathiriwa na mvua za El-Nino.

Bashungwa aliyasema hayo juzi jioni bungeni wakati akijibu hoja mbalimbali za wabunge waliokuwa wakijadili makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

"Wakati wa Bunge la Februari tulifanya tathimini ya uharibifu wa miundombinu na hasara ilikuwa ni Sh. bilioni 200, lakini mpaka jana miundombinu mingi imeharibika na ili tuweze kuirudisha tunahitaji Sh. bilioni 500 (nusu Trilioni)", alisema Bashungwa.

Bashungwa alisema kuwa kiasi hicho cha fedha kinachohitajika ndicho kingeweza kupelekwa kwenye miradi ya barabara iliyopo katika hatua mbalimbali za ujenzi kwa kiwango cha lami, barabara ambazo zimeshasainiwa na zile ambazo zipo katika hatua za manunuzi.

"Kutokana changamoto ya mvua za El-Nino zinazoendelea kunyesha kupita kiasi, Wizara italazimika kujipanga upya kurejesha miundombinu hiyo ili kuhakikisha Watanzania wanaendelea kuwa na mawasiliano ya barabara, huku tukiendelea na mkakati wa kudumu wa kuzijenga kwa kiwango cha lami", alisema Bashungwa.

Aidha, Bashungwa alieleza kuwa kila mwaka Serikali inatumia takribani kiasi cha Sh. bilioni 550 kwa ajili ya kufanya matengenezo ya barabara za kiwango cha changarawe hapa nchini.

Vilevile, Bashungwa alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuiwezesha TANROADS na TARURA kuendelea kuweka jitihada za kurudisha mawasiliano pale yanapoharibika.

Kuhusu utekelezaji wa miradi hapa nchini, Bashugwa alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitatu ya Serikali imefanikiwa kukamilisha ujenzi wa barabara 25 kwa kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 1,198.5 na madaraja makubwa nane.

Bashungwa alisema kuwa Serikali inaendelea na utekelezaji wa madaraja matano ambayo yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi na inaendelea na ujenzi wa barabara 57 kwa kiwango cha lami ambapo zikikamilika Serikali itakuwa imejenga barabara zenye kilometa 3,794.

Pia, Bashungwa amebainisha kuwa miradi ya barabara 49 ipo katika hatua za kusainiwa mikataba na miradi ya barabara 30 ipo hatua za manunuzi.



Baadhi ya wakuu wa mikoa wakiwa eneo la wageni walipofika hapo kusikiliza hotuba ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), iliyowasilishwa na Waziri wa Wizara hiyo, Mohamed Mchengerwa (hayupo pichani), Bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wasichana 178,114 kupata chanjo saratani mlango wa kizazi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WASICHANA 178,114 wenye umri kati ya miaka 9 hadi 14 mkoani Singida wanatarajia kupatiwa chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi, ili kujikinga na maambukizi ya virusi vinavyosababishwa na ugonjwa huo.

Mratibu wa huduma za chanjo Mkoa wa Singida, Jadili Mhanginoma, aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha uhabarisho ngazi ya mkoa kilichowajumuisha wakuu wa wilaya, wakurugenzi wa halmashauri, viongozi wa dini, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Singida na wataalamu wa afya kutoka wilaya zote za mkoa.

Alisema chanjo hiyo itaanza kutolewa Aprili 22 hadi 26, 2024 kwa wasichana wote wenye umri wa miaka 9 hadi 14, kwamba katika kuhakikisha chanjo inafanikiwa mkoa umepokea chanjo dozi 191,940 na usambazaji kwenda ngazi ya halmashauri unaendelea.

Mhanginoma alisema hali ya utoaji chanjo kwa Mkoa wa Singida katika kipindi cha mwaka 2018 hadi 2024 waliopata dozi ya kwanza walikuwa 131,677, dozi ya pili 96,932 na ambao hawakukamilisha dozi ya pili walikuwa 34,745.

"Chanjo ya saratani ya mlango wa uzazi nchini iliidhinishwa na Shirika la Afya Dunia (WHO) na Wizara ya Afya kupitia Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) mwaka 2014 ambapo ilianza kutolewa katika Mkoa wa Kilimanjaro na mwaka 2018 ilianza kutolewa nchi nzima," alisema.

Mhanginoma alisema chanjo hiyo inatolewa kwa wasichana kutokana na sababu za kibailojia na kiuchumi ambapo wanawake huathiriwa zaidi na maambukizi ya virusi, hivyo kuwakinga kutapunguza maambukizi kwa wanaume kwasababu ugonjwa huo unaambukizwa kwa njia za kujamiana.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, aliwataka viongozi mbalimbali wakiwamo viongozi wa dini kuwaelimisha wazazi wenye watoto wa kike wenye umri kati ya miaka 9 hadi 14 kuwapeleka kupata chanjo ya saratani ya mlango wa kizazi.

Alisema Serikali imeweka mikakati ya kuhakikisha wanawake wanapewa chanjo hiyo lengo kuwafanya wanapofikia umri wa kuwa 'active' katika masuala ya kujamiana wawe na kinga hasa kutokana ugonjwa huu unaambukiza kirahisi kwa njia ya kujamiana.

"Tumeitana kama wajumbe wa kamati na kama viongozi kweye jamii tunajua jamii zetu zina mitazamo tofauti na tunaishi kwenye mila na desturi tofauti, lakini hili lazima tuungane sote kwasababu madhara ya ugonjwa huu yanatuathiri sisi wote bila kuangalia tofauti ambazo tunazo," alisema.

Dendego alisema ili kuweza kufanikisha chanjo hii viongozi wote ambao wana ushawishi mkubwa kwenye jamii wasaidie kuwahamisha wazazi ambao wana wasichana wenye umri wa kuanzia miaka 9 hadi 14 kuhakikisha wanapata chanjo ya saratani ya mlango wa uzazi.

Dendego alisema chanjo hiyo ilianza kutolewa mwaka 2018, wale ambao wakipata chanjo kipindi hicho wawe wanashirikishwa kwenye zoezi la kuhamasisha wengine.





# Mtoto mbaroni kwa kumlawiti mwenzie

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linamshikilia mtoto wa umri wa miaka 12 kwa tuhuma za kumlawiti mtoto mwenzake, mwanafunzi wa shule ya msingi iliyopo Halmashauri ya Mji wa Makambako wilayani Njombe.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Mahamoud Banga aliwambia waandishi wa habari kuwa tukio hilo lilitokea Aprili 4, mwaka huu katika Mtaa wa Jeshini Kata ya Maguvani ya halmashauri hiyo.

Alisema inadaiwa kuwa mwanafunzi huyo (10) alikuwa akilawitiwa mara kwa mara na mtuhumiwa huyo kwa ahadi ya kupewa fedha.

"Mtuhumiwa huyu anaonekana aliacha shule akiwa darasa la sita, lakini amekuwa akimfanyia mwenzake hivi vitendo kwa muda mrefu kwa ahadi ya kumpatia fedha," alisema Banga.

Alisema kwa muda wote huo, mwanafunzi huyo hakusema kwa wazazi kuwa alikuwa akifanyia vitendo hivyo, lakini tabia yake ilianza kubadilika baada ya kuanza kutokwa kinyesi.

Kamanda huyo, alisema baada ya mama yake kugundua hali hiyo na kumuadhibu, alimueleza kuwa alikuwa anafanyiwa vitendo hivyo na mtuhumiwa huyo.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri hiyo, Masinde Masinde, alisema matukio ya ulawiti kwa sasa yamekuwa mengi, hivyo wazazi wanatakiwa kuwa karibu na watoto wao ili kuwalinda.

"Niwaombe wazazi watimize jukumu lao la malezi kwa watoto ili kuwalinda katika suala zima la ukatili hasa huu uliokithiri wa ubakaji na ulawiti," alisema Masinde.

Balozi wa Mtaa wa Jeshini, Charles Mkane, aliiomba serikali kuwachukulia hatua za kali watu wanaojihusisha na vitendo vya ulawiti kwa kuwa vimekuwa vikikithiri siku hadi siku katika jamii.

Mzazi wa mtoto ambaye inadaiwa kufanyiwa vitendo hivyo, alisema alibaini changamoto hiyo baada ya kuona kila anapofua nguo zake zina uchafu wa haja kubwa.

"Nimekutwa na changamoto ya ukatili kwa mwanangu na amefanyiwa na mtoto mwenzake kwa kulawitiwa kwa muda mrefu," alisema mzazi huyo.



Gari likipita katika dimbwi la maji eneo la Ukonga Majumba Sita, jijini Dar es Salaam jana. Mvua inayoendelea kunyesha imesababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu ya barabara. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Waua mlinzi, waiba fedha, vocha

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

WATU tisa wanashikiliwa na Jeshi la Polisi Mkoa wa Njombe kwa tuhuma za mauaji ya mlinzi, Samwel Nofola (28), Mkazi wa Kijiji cha Mtewele kilichopo Kata ya Uhambule wilayani Wanging'ombe mkoani hapa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa huo, Mahamoud Banga alisema kuwa tukio hilo lilitokea katika Mtaa wa Uzunguni uliopo Kata ya Maguvani Halmashauri ya Mji wa Makambako usiku wa kuamkia Aprili 13, mwaka huu.

Banga alisema kuwa Nafola akiwa mwajiriwa wa kampuni ya ulinzi iliyopo mjini Makambako, watu wasiojulikana walimvamia na kumuua, kisha kuvunja maduka manne na kuiba vitu mbalimbali.

Alivitaja vitu vilivyoibiwa kwenye maduka hayo kuwa mafuta ya kula lita sita na nusu, vocha ambazo gharama yake haizidi 70,000 , sabuni na manukato.

"Kuna mfanyabiashara mmoja ambaye ni mwalimu yeye alidai ndani ya duka lake kulikuwa na Sh. 300,000 hakuzikuta lakini mwingine 2,000 za chenji ukichanganya na vitu vilivyochukuliwa unapata Sh. 500,000 lakini utaona hapo uhai wa mtu umetolewa," alisema Banga.

Alisema huenda mauaji hayo yalikuwa ni kulipiza kisasi na kuhoji kama lengo lilikuwa kuiba mali zenye thamani ndogo kiasi hicho kipi kimewafanya watuhumiwa hao kutoa uhai wa mtu.

Kamanda huyo, alisema kijana huyo aliyeuawa alikuwa akiishi wilayani Wanging'ombe, jioni alikuwa anakwenda kufanya kazi zake Makambako ambako aliajiriwa na kurudi tena nyumbani kwake.

"Mpaka sasa watu tisa tunawashikilia kuhusika na tukio hilo na tunaendelea na mahojiano huku uchunguzi zaidi ukiendelea kufanyika," alisisitiza kamanda huyo. Alitoa wito kwa wafanyabiashara na kampuni za ulinzi kuacha kuweka mlinzi mmoja kwa ajili ya kulinda maduka mengi kwenye eneo kubwa kwa sababu inawawia vigumu kuhimili endapo kutatokea changamoto ya kuvamiwa na watu wasiojulikana kwa nia ovu.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Uzunguni, Yusto Kiyeyeu alisema tukio hilo la mauaji ni la ajabu kwani halijawahi kutokea kwenye mtaa huo kuhusisha mlinzi.

"Sasa hivi kumekuwa na vibaka ndani ya mtaa wangu na wengine wanashirikiana kutoka mitaa mingine," alisema Kiyeyeu.

Wafanyabiashara waliovunjiwa maduka yao na kuibiwa fedha na bidhaa zao akiwemo Christina Kilindila na Martin Nzalalila walielezea kusikitishwa na tukio hilo.

"Tukio linasikitisha unaiba vitu halafu unaua mlinzi kwakweli dunia inaelekea kubaya," alisema Kilindila.

# Walimu wapewa mbinu kuongeza ufaulu

**Na Elizabeth John,** MAKETE

WALIMU wametakiwa kuacha kufundisha kwa mazoea ili kuleta matokeo chanya kwa wanafunzi wao na kuongeza kiwango cha ufaulu wilayani hapa Mkoa wa Njombe.

Wito ulitolewa na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, William Makufwe kwenye mahafali ya 46 ya Chuo cha Ualimu Tandala kilichopo wilayani hapa.

Mafukwe, alisema kuna changamoto ya walimu kufanya kazi ya kufundisha kwa mazoea na kuchangia wanafunzi kufanya vibaya katika mitihani yao ya mwisho.

Alisema wanafunzi wengi inapokuja mitihani wanafeli na hata wanaofaulu ni wachache katika kiwango ambacho hakiridhishi.

"Sasa nyinyi wahitimu wa leo mtakapopangiwa vituo vya kufanyia kazi naomba mkawe chachu ya mabadiliko kwenye shule mtakazopangiwa," alisema Makufwe.

Aliwataka wahitimu hao kutanguliza nidhamu na kujituma na kuwa wa kwanza kukemea wanapoona jambo linaharibika ili wawe mabalozi wazuri wa chuo hicho.

Mkuu wa Chuo hicho, Vedasto Kibyala, alisema chuo chao kimeongoza kitaifa katika mitihani ya kuhitimu kwa miaka mitatu mfululizo kwa wanafunzi wao kufaulu kwa asilimia 100.

Kibyala, alisema mwaka jana walikuwa na wanachuo 185, kati yao 27 walipata alama ya juu kabisa ya ufaulu na kuongoza kitaifa katika mitihani.

"Chuo chetu kimejipambanua kuhakikisha kinawafundisha walimu bora, kuwaandaa na kuwasimamia ili kuhakikisha mtaala unavyoelekeza wanafundishwa," alisema Kibyala.

Mwenyekiti Bodi ya Chuo hicho, Jassery Mwamwala, alisema chuo kinawaandaa walimu kuwa bora kulitumikia taifa lao.

"Pamoja na kuwa tunataka wakajitegemee, nia ya sisi wazazi ni kuwa wawe na ajira, tulikuwa tunafikiri ni vizuri tunapopika vijana hawa na ajira ziwepo," alisema Mwamwala.

Mmoja wa wahitimu hao, Majaliwa Mungo, alisema elimu waliyopata watatumia kulingana na mazingira watakayokuwa ili kuinua kiwango cha elimu nchini.

"Walimu wengi wamezoea kufundisha kwa kuchukua kitabu na kwenda nacho darasani kufundisha aangalii wahitaji waliopo darasani wanataka kutumia nini," alisema Mungo.





## Wizara yaazimia kutokomeza ugonjwa wa malaria

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema itaendeleza jitihada ya kupambana na ugonjwa wa malaria na kuhakikisha kuwa unaondoka visiwani hapa.

Waziri wa wizara hiyo, Nassor Ahmed Mazrui, aliyasema hayo alipofanya mazungumzo na Balozi Maalumu wa Taasisi ya African Leaders Malaria Alliance (ALMA), Anthony Okaraa aliyefika ofisini kwake Vuga kwa mazungumzo.

Alisema Wizara ya Afya kwa kushirikiana na washirika wa maendeleo wanafanya jitihada za makusudi malaria yanaondoka kabisa ambapo tayari zipo nchi nne kwa Afrika zimefikia kiwango cha kundoa ugonjwa huo.

Alisema Zanzibar ikiwa nchi inayotegemea utalii na nguvu kazi ya wananchi, hivyo ni muhimu sana kuona kuwa ugonjwa wa malaria yanaondoka kama nchi nyingine walivyofanikiwa katika kuutokomeza.

Alisema wizara kupitia programu ya kumaliza ugonjwa wa malaria wanafanya kazi pamoja na Taasisi ya ALMA, hivyo ujio wa balozi huyo ni kutaimarisha ushirikinao uliopo.

Alisema katika maadhimisho ya mwaka huu wamejipangia kufanya mambo mbali mbali ikiwemo ugawaji wa vyandarua nchi nzima.

Katika kufikia mpango mpya wa kupambana na malaria, Mazrui aliwata wananchi kushiriki kikamilifu katika juhudi za kutokomeza ugonjwa huo, akisema Baraza la Umoja wa Malaria Zanzibar litaundwa kwa kushirikisha mashirika, Serikali, taasisi zisizo za kiserikali na wananchi.

Alisema mpango huo umefanikiwa katika kuondosha ugonjwa wa malaria katika nchi mbalimbali.

Balozi Okaraa alisema wataendeleza ushirikiano na Zanzibar katika kupambana na ugonjwa wa malaria ili maradhi hayo yanaondoka hapa nchini.

Alisema kuwa Zanzibar inafanya jitihada za kuondosha ugonjwa huo, hivyo taasisi hiyo itaunga mkono jitihada hizo ili ugonjwa wa malaria usiwe tatizo katika visiwa vya Unguja na Pemba.

# Serikali: Mitaala mipya ya elimu italeta mageuzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Muhammed Mussa amesema utekelezaji wa mitaala mipya ya elimu itatengeneza msingi madhubuti wa kufika malengo ya mageuzi ya mifumo ya elimu nchini.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa saba wa tathmini ya sekta ya elimu visiwani hapa.

Alisema utekelezaji wa mitaala pamoja na dhama nzima ya mageuzi inahitaji miundombinu ya kisasa na ya kutosha.

Waziri Lela alisema kwa kulitambua hilo na kwa kuzingatia changamoto ya msongamano wa wanafunzi kwa darasa moja na uendeshaji wa shule, serikali imedhamiria kuondosha kadhia hiyo ili watoto wapate elimu katika mazingira bora.

Aidha, alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Hussein Ali Mwinyi, serikali imefanikiwa kujenga madarasa 2,273 pamoja na vyoo 2,189.

Alisema sambamba na ujenzi wa madarasa serikali pia imejenga maabara na nyumba za walimu ambapo kasi hiyo ya uimarishaji wa miundombinu itasadia kuondokana na changamoto ya msongamano wa wanafunzi madarasani.

"Serikali imefanikiwa kujenga ofisi maalum za walimu za wilaya ambapo jumla ya ofisi saba zimejengwa na imepanga kumaliza ofisi nne ili kila wilaya kuwa na ofisi"alisema.

Alisema wakati juhudi za uimarishaji wa miundombinu zikiendelea serikali nayo ipo katika hatua za mwisho za ukamilishaji wa mpango wa utekelezaji wa mageuzi ya elimu unaotekelezwa kwa kipindi cha miaka saba hadi mwaka 2030.

Alisema kukamilika kwa mpango huo kutatoa fursa ya kufuatilia kwa ufanisi utekelezaji wa mapendekezo waliyokubaliana katika mkutano wa sita wa tathmini ya elimu.

Hata hivyo, alisema serikali imetoa mkazo kuhusu uimarishaji wa ujuzi kwa wanafunzi, hivyo suala la elimu ya ufundi na mafunzo ya amali litakuwa na nafasi kubwa katika utekelezaji wa mpango huo.

Alisema serikali inatambua kuwa pamoja na kuwa na mpango huo, ni lazima mchakato wa mapitio wa sera na sheria ya elimu uwe umekamilika ili kuandaa mazingira bora ya utekelezaji.

Naye Katibu Mkuu Wizara hiyo, Khamis Abdallah Said, alisema wizara itahakikisha inaendeleza mikutano ya tathmini inayofanyika kila mwaka, ili kufanikisha sekta ya elimu kupata maendeleo zaidi.

Aidha, alisema katika kufanikisha tathmini ya elimu wizara imefanikisha wadau kuzitembelea taasisi mbalimbali ikiwemo shule ili kutathmini sekta hiyo ambapo taasisi 24 zimetembelewa Unguja na Pemba.

Alisema kuwa wizara hiyo inaendelea kutekeleza maagizo ya Rais kuunga mkono juhudi za wadau kufanikisha sekta ya elimu nchini.

Mwenyekiti Mtandao Elimu kwa wote Zanzibar, Salim Ali Sali, alipongeza Serikali kuthamini juhudi za asasi za kiraia kwa lengo la kuhakikisha sekta ya elimu inaimarika.

Aidha, aliitaka serikali kuekeza fedha za kutosha katika bajeti ya mwaka ujao sambamba na kuondoa tozo ya kibiashara katika sekta binafsi ya elimu ili kusaidia kutimiza wajibu wake katika huduma ya kutoa elimu.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Zanzibar Milele Foundation, Khadija Ameir Sharif, alisema serikali imechangia kwa kiasi kikubwa kujenga miundombinu rafiki ya ufundishaji, hivyo inapaswa kuweka kipaumbele kwa walimu.




Katibu Mkuu wa Shirika la Viwango Afrika (ARSO), Dk. Hermogene Nsengimana (kulia), akimsikiliza Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya viwango Zanzibar (ZBS), Yussuph Majid Nassor alipofanya ziara Zanzibar jana, kukagua maendeleo ya taasisi hiyo na maandalizi ya mkutano mkuu wa mashirika ya viwango Afrika utakaofanyika kisiwani humo, mwakani. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Maendeleo ZBS yamkosha bosi ARSO

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Shirika la Viwango Afrika (ARSO), Dk. Hermogene Nsengimana ameridhishwa na maendeleo yaliyofikiwa na Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS) toka ilipojiunga na shirika hilo kama mwanachama mwangalizi.

Dk. Nsengimana alisema hayo juzi alipotembelea ofisi za taasisi hiyo zilizopo Maruhubi na kukagua baadhi ya maabara pamoja na kuzungumza na uongozi wa taasisi hiyo.

Dk. Nsengimana amefanya ziara hiyo ikiwa ni sehemu ya ziara yake nchini kukagua maandalizi ya mkutano mkuu wa mashirika ya viwango Afrika unaotarajiwa kufanyika mwakani.

Alisema kuwa taasisi hiyo imekuwa na mafanikio makubwa kwa kuongeza idadi ya maabara na kuweka mifumo imara ya ukaguzi kiasi cha maabara ya uchunguzi wa bidhaa za kemikali kupata alama ya ithibati ya taassi ya udhibiti ubora kwa nchi za Ukanda wa Kusini mwa Afrika.

"Nimefurahi kuona ZBS inaendelea kuimarika na kuna ongezeko la maabara. Hii ni hatua muhimu kwa taasisi yenye dhamana kubwa kama hii, hivyo ni vyema kama shirika linalosimamia mashirika ya viwango barani Afrika tujivunie hatua iliyofikiwa", alisema Dk. Nsengimana.

Aidha, aliwataka watendaji wa taasisi hiyo kuendelea kusimamia miongozo na makubaliano ya kikanda na kimataifa wanaposhughulikia uthibitishaji wa viwango wa bidhaa, ili kulinda hadhi ya bidhaa zinazozalishwa au kuingizwa nchini.

Akizungumzia mkutano mkuu wa ARSO, Dk. Nsengimana alisema amefurahishwa kuona kuna ushirikiano katika maandalizi ya mkutano huo kati ya wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania zinazosimamia taasisi za viwango nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa ZBS, Yussuph Majid Nassor, alisema wamefarajika kutembelewa na kiongozi huyo ambaye aliambatana na Mratibu wa Miradi wa Shirika hilo, Sandra Umugwaneza.

Alisema taasisi imepata fursa ya kuainisha mambo mbali mbali ambayo yatawasilishwa katika vikao vya ARSO kabla ya mkutano mkuu ambao utafanyika Zanzibar.

Aidha, alisema kuwa ziara ya kiongozi huyo iliyoanzia Tanzania Bara kwa kukutana na viongozi mbalimbali wakiwemo wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) imekuja wakati muafaka ambapo taasisi hiyo ipo katika mchakato wa kukamilisha maabara tano mpya ikiwemo ya bidhaa za ujenzi.

## Watu 40 wauawa kwa mvua, radi

**BALOCHISTAN,** Pakistan

TAKRIBAN watu 39 wameuawa nchini Pakistan, baada mvua kubwa kunyesha kusini magharibi mwa nchi hiyo, kwa siku kadhaa.

Baadhi ya waliouawa walikuwa wakulima waliopigwa na radi wakati wakivuna ngano, mamlaka ilisema.

Picha mtandaoni zinaonyesha maeneo mengi ya mashamba yaliyosombwa na maji ya mvua.

Mafuriko makubwa pia yametatiza usambazaji wa umeme na miundombinu ya usafirishaji.

Pakistan imeshuhudia ongezeko la matukio ya hali ya hewa kali, ambayo inakabiliana na athari za mabadiliko ya hali ya hewa.

Mwaka 2022, theluthi moja ya nchi ilisombwa kabisa na mafuriko, ambayo hayajawahi kutokea na kuua zaidi ya watu 1,700 na kujeruhi maelfu wengine.

Mamilioni waliachwa bila makao na kukosa maji safi ya kunywa, kwa miezi kadhaa baadaye.

Baadhi ya maeneo yaliyoathiriwa na mafuriko ya mwaka 2022, ni pamoja na Khyber Pakhtunkhwa na Balochistan, yameathiriwa tena na dhoruba za hivi majuzi.

Huku mvua zaidi ikitarajiwa katika siku zijazo, Mamlaka ya Kitaifa ya Kukabiliana na Majanga ya Pakistan, pia imeonya kuhusu maporomoko ya ardhi na mafuriko makubwa.

**BBC**

## Afrika yahofia dawa ya kikohozi

**NAIROBI,** Kenya

MATAIFA ya Tanzania, Rwanda na Afrika Kusini yamejiunga pamoja na Kenya na Nigeria, kusitisha matumizi ya dawa ya kikohozi kwa watoto kwa jina Benylin.

Hii ni kutokana na wasiwasi kuhusu usalama wake, baada ya vipimo vya maabara nchini Nigeria, kubaini kuwa dawa hizo za kikohozi za kampuni ya Johnson & Johnson zilikuwa na sumu.

Dawa hiyo ina kiungo ambacho uchunguzi umebaini kwamba, kilisababisha vifo vya watoto nchini Gambia, Uzbekistan na Cameroon, tangu mwaka 2022.

Kemikali ya Diethylene glycol ni sumu kwa binadamu inapotumiwa na inaweza kusababisha figo kushindwa kufanya kazi.

Dawa ambazo zimepigwa marufuku zilitengenezwa nchini Afrika Kusini, mwaka 2021 na zinatarajia kupitisha muda wake wa matumizi mwezi huu wa April, mwaka 2024.

Bodi ya DSawa nchini Kenya, imesema ya kwamba imeanzisha uchunguzi huku ikiwataka wananchi walionunua dawa hizo, kuzirejesha mara moja.

**BBC**

# Wafadhili wa kimataifa waahidi dola bilioni 2.1/- kwa Sudan

**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amesema wafadhili wa dunia wameahidi dola bilioni 2.1 ili kusaidia kukabiliana na mgogoro wa kibinadamu ulioko nchini Sudan.

Macron, akiwa mjini Paris kwenye mkutano wa kimataifa, kuhamasisha umuhimu wa msaada wa kifedha, kwa juhudi ambazo ufadhili wake umepungua kwa kiasi kikubwa.

Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa (UN), Antonio Guterres, aliitaka dunia kutosahau kuhusu watu wa Sudan, huku akitoa wito wa kusitishwa kwa mapigano katika maadhimisho ya mwaka mmoja wa vita vya wenyewe kwa wenyewe vya taifa hilo.

"Ni vita dhidi ya maelfu ya raia ambao wameuawa, na dazani za maelfu ya watu waliojeruhiwa," aliwaambia waandishi wa habari katika makao makuu ya UN, huko NewYork.

"Ni vita dhidi ya watu milioni 18 wanaokabiliwa na njaa kali na jamii sasa zinatazamia tishio la njaa katika miezi ijayo."

Mapigano yalizuka katika mji mkuu, Khartoum, mwaka mmoja uliopita kati ya majenerali wapinzani, mmoja akiongoza Kikosi cha Wanajeshi wa Sudan (SAF) na mwingine Kikosi cha RSF.

Uadui ulienea haraka nchi nzima.

Umoja wa Mataifa, unasema zaidi ya watu milioni nane, wamekimbia makwao kutafuta usalama na kati yao, milioni 1.8 wamehamia nchi jirani.

Jitihada za kuwasaidia mamilioni ya watu wanaokabiliwa na njaa kutokana na vita zimezuiliwa na kuendelea kwa mapigano yanayoendelea na vikwazo vilivyowekwa na pande zinazopigana.

Hali hiyo inaathiriwa pia na ukosefu wa ufadhili wa kutosha kutoka kwa jumuiya ya kimataifa, kutokana na mataifa mbalimbali pia kuhitajika kufadhili migogoro mingine ya kimataifa, ikiwa ni pamoja na Gaza na Ukraine.

**VOA**



Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron **PICHA: MTANDAO**

## OPEC+ yaikaribisha Namibia mwanachama mpya

**VIENNA,** Austria

KUNDI la mataifa yanayozalisha mafuta la OPEC+, limeikaribisha Namibia kujiunga katika umoja huo.

Hatua hiyo inakuja baada ya kupoteza uanachama wa Angola, miongoni mwa wengine katika miaka ya karibuni.

Hilo limefanyika wakati taifa hilo, likijianda kuwa mzalishaji wa nne kwa ukubwa barani Afrika, ndani ya muongo mmoja ujao.

Makampuni ya mafuta ya TotalEnergies na Shell katika miaka ya karibuni, yamegundua mafuta yanayokisiwa kuwa mapipa bilioni 2.6 nchini humo. Angola, inapanga kuanza uzalishaji wa mafuta ya kibiashara ifikapo 2030.

Taarifa zimeongeza kuwa lengo kubwa la OPEC+ kwa sasa, ni kuikaribisha Namibia kwenye mkataba wa ushirikiano, ambao utafungua milango ya mazungumzo ya muda mrefu kuhusu soko la mafuta.

Brazil ilijiunga kwenye mkataba huo, Januari mwaka huu.

Wakati huo huo, bei ya mafuta imepanda siku ya jana, huku uchumi wa China ukikua kwa kasi zaidi kuliko ilivyotarajiwa.

Hata vivyo hali ya wasiwasi katika Mashariki ya Kati, inaendelea kuweka soko kwenye msukosuko mkali, baada ya Israel kusema kuwa itajibu shambulio la wikendi la Iran, dhidi yake.

Bei ya mafuta ghafi nchini Marekani kwa usambazaji wa Mei, ilipanda kwa senti 49 au asilimia 0.6 hadi dola 85.90 kwa pipa.

Vigezo vilipanda juu ya ukuaji thabiti wa uchumi nchini China, mwagizaji mkuu wa mafuta duniani.

Pato la taifa lilikua asilimia 5.3 katika robo ya kwanza, mwaka baada ya mwaka, data ya serikali ilionyesha na kushinda matarajio ya wachambuzi.

Iran, inazalisha zaidi ya mapipa milioni tatu, kwa siku mafuta ghafi kama mzalishaji mkuu ndani ya Shirika la Nchi Zinazouza Petroli (OPEC).

**VOA/BBC**

# SIMBA SC, YANGA ZANOGESHA MTOKO WA KIBINGWA NCHINI

**Mwandishi Wetu**

WAKATI homa ya mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga ikiongezeka, mashabiki wa timu hizo wameendelea kunogesha Kampeni ya 'Mtoko wa Kibingwa' inayoendelea kote nchini.

Kampeni hiyo inatoa fursa kwa mashabiki 56 kuishuhudia mubashara mechi hiyo ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara Yanga ikiwa mwenyeji, ambayo itapigwa Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkaka, Dar es Salaam.

Mashabiki wa timu hizo kwa nyakati tofauti wamekuwa wakitambiana huku uhondo zaidi ukiwa kwenye Kampeni ya Mtoko wa Kibingwa inayowapa fursa kuishuhudia dabi hiyo mubashara kwa hadhi ya VIP.

Mbali na kuishuhudia mechi hiyo, gharama zote hulipIwa na Kampuni ya Michezo ya Kubashiri Matokeo ya Betika, pia washindi wawili wa kampeni hiyo wamepewa zawadi ya iphone 15 katika droo hiyo.

Balozi wa kampeni hiyo, msimu huu, Baraka Mpenja, juzi alimkabidhi iphone mshindi wa pili wa droo hiyo, Jackson Lazaro, kutoka Morogoro, ambapo alisema ni miongoni mwa washindi wawili wa kila mwezi wa iphone 15 kwenye kampeni hiyo inayofanyika kila mwaka huku mwingine akiwa ni Peter Longolongo wa Gongo la Mboto, Dar es Salaam.

"Hawa ndio washindi wetu wa Machi na Aprili wa kampeni hii ya Mtoko wa Kibingwa ambayo pia inawapa fursa mashabiki 56 kuishuhudia dabi kwa gharama za Betika," alisema.

Awali, Ofisa Habari wa Betika, Juvelinaus Rugambwa, alisema mbali na zawadi hizo za mwezi, pia kulikuwa na washindi wawili kila wiki wa simu janja aina ya Tecno.

"Kampeni imefanyika kwa miezi miwili, tukielekea kwenye dabi huku mabingwa wetu wa Mtoko wa Kibingwa nao wakiendelea kumiminika," alisema.

Rugambwa alisema washindi kutoka nje ya Dar es Salaam watawasili siku moja kabla ya mechi hiyo ya dabi kwa ndege na wataungana na wale wa Dar es Salaam tayari kuishuhudia dabi hiyo.

"Kila wiki tumekuwa na washindi wanane, lengo ni kuwapa fursa mashabiki wa Simba na Yanga kuishuhudia dabi hiyo mubashara kwa hadhi ya VIP kwa gharama za Betika.

"Kama kawaida yetu Betika, washindi wote watalala kwenye hoteli ya nyota tano, watakwenda kwa king'ora uwanjani na kukaa jukwaa kuu la VIP," alisema.

Akizungumzia kampeni ya Mtoko wa Kibingwa, Rugambwa alisema tangu imeanza imeweza kuwaleta mashabiki 350 kushuhudia dabi hiyo.

"Wengi hawakuwa wamewahi kuishuhudia dabi hiyo mubashara, jambo hili limewakutanisha na wachezaji wanaowapenda na kuwaona 'laivu' wakicheza. Betika kwa kutambua uhitaji huo, msimu huu tumeongeza idadi ya washindi ili kuwapa fursa zaidi kuishuhudia dabi hiyo," alisema.




Mshindi wa Iphone 15 kwenye kampeni ya Mtoko wa Kibingwa, Jackson Lazaro (kushoto), kutoka Morogoro akikabidhiwa zawadi hiyo jijini Dar es Salaam jana na Balozi wa Betika, Baraka Mpenja. Mpigapicha Wetu **PICHA: MTANDAO**

# New City FC lengo kubaki Ligi Kuu

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

UONGOZI wa New City FC, umesema mikakati yao mikubwa ni kuhakikisha timu hiyo inafanikiwa kuendelea kuwapo Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

New City FC huu ni msimu wake wa kwanza kucheza Ligi Kuu, lakini hajafanya vizuri kama ilivyotarajiwa na mashabiki wake.

Akizungumza na gazeti hili jana, mmoja wa viongozi wa timu hiyo, Razak Salum Rajabu 'Wenger', ambaye anakinoa kikosi hicho katika mazoezi, alisema mpango wao mkubwa uliopo ni kuhakikisha timu inasalia Ligi kuu Zanzibar.

Alisema michezo kumi iliyobakia watajitahidi kupambana ili kupata alama ambazo zitaisogeza timu hiyo katika nafasi za juu za msimamo wa Ligi Kuu.

Wenger alisema katika kuhakikisha timu yao inatimiza lengo lao hilo, tayari wameshafanya maandalizi ya mapema ikiwamo wachezaji wote kuingia kambini ili kupata mtiririko mzuri wa mazoezi ya pamoja.

"Ligi bado ngumu na michezo 10 iliyobakia ni migumu sana maana kuna zile zinazotaka ubingwa na zinazotaka kubaki Ligi Kuu, hivyo lazima tupambane tuizuie timu ibaki Ligi Kuu," alisema.

Aidha, alisema anaamini wachezaji wake wanaonesha uwezo mzuri kama walivyofanya katika michezo mitano ya mwisho kabla ya kusimama kwa ligi.

"Kikosi chetu kimebadilika sehemu kubwa tofauti na tulivyoanza ligi, hivyo imani yangu na maandalizi tuliyoyanya wachezaji watabadilika zaidi na kufanya vizuri kama tulivyokusudia," alisema.

Hata hivyo, aliwaomba mashabiki wa timu hiyo kutovunjika moyo katika kuipa hamasa timu yao kutokana na matokeo waliyokuwa wakiyapatia michezo iliyopita badala yake wajitokeze kwa wingi katika michezo hii ya kumalizia msimu.

New City FC ipo nafasi ya 12 ikiwa na alama 22 baada ya kushinda michezo mitano, sare saba na kupoteza mechi nane katika michezo 20 iliyocheza.

## Isanzu, Kadio wang'ara gofu kumuenzi Lina

**Na Mwandishi Wetu**

MCHEZA gofu wa ridhaa kutoka Klabu ya TPC mkoani Kilimanjaro, Ally Isanzu na mchezaji wa gofu wa kulipwa kutoka Dar es Salaam, Hassan Kadio, wameibuka vinara wa raundi ya pili ya michuano ya gofu ya Lina PG yaliyomalizika hivi karibuni mjini Morogoro.

Licha ya ushindi wao ambao unawaweka katika nafasi nzuri ya kukata tiketi ya kucheza michuano ya kimataifa itakayofanyika Falme za Kiarabu hivi karibuni, mabingwa hao pia walizawadiwa donge nono la fedha kwa ushindi wao.

Kadio ambaye alikuwa mshindi wa kwanza katika mashindano hayo alijizolea kitita cha Sh. milioni 6.8 huku Isanzu akiondoka na Sh. milioni mbili kama mshindi wa gofu ya ridhaa.

Licha ya kuwa bora katka kitengo cha ridhaa, Isanzu ndiye alikuwa na matokeo bora zaidi katika michuano hiyo baada kupata mikwaju 74, 73, 72 na 78 katika siku nne za michuano ambayo ilipitia mashimo 72.

Isanzu alimaliza na matokeo ya jumla ya +9 na kufuatiwa na Kadio mwenye matokeo ya +12, huku mchezaji Abddalah Yusuf aliyepata jumla ya alama +16, alikuwa wa pili kwa wachezaji wa kulipwa mbele ya mshindi wa tatu, Nuru Mollel aliyepata alama +17.

Bryszon Nyenza ambaye alimaliza na alama +18 alikuwa wa nne wakati nafasi ya tano ikienda kwa Isack Wanyeche aliyerudisha alama +22

Washindi watakaokwenda Dubai ni wale wenye matokeo mazuri ya jumla baada ya kumalizika kwa raundi ya tano ya mashindano hayo.

Baada ya raundi ya pili ya Morogoro, Arusha Gymkhana sasa itakuwa ni mwenyeji wa raundi ya tatu na kwa mujibu wa Mkurugenzi wa michuano hiyo, Yasmin Challi, alisema kuwa raundi ya tatu itachezwa Julai mwaka huu.

Alisema wachezaji wengine katika kiwango cha kumi bora walikuwa ni Fadhil Nkya, Frank Roman, Salum Dilunga Ninja, na Athumani Chiundu.

## ZISIKUPITE

### AIT-NOURI ATAKIWA CITY
KLABU ya Manchester City imeanza mazungumzo na Wolves kuhusu uwezekano wa kumsajili winga wa Algeria, Rayan Ait-Nouri (22). (***Footyball Transfer***)

### ADARABIOYO ATAKIWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur imetoa ofa kwa Tosin Adarabioyo wa Fulham wakati wakijaribu kuishinda Manchester United katika mbio za kumnunua beki huyo wa England mwenye umri wa miaka 26. (***Teamtalk***)

### NEWCASTLE NAO WAMFUKUZIA
KLABU ya Newcastle United inaangalia uwezekano wa kumsajili Tosin Adarabioyo pamoja na mlinzi wa kati wa Bournemouth, Lloyd Kelly mwenye umri wa miaka 25, kwani wawili hao wanamaliza mikataba yao msimu ujao. (***Telegraph***)

### GYOKERES AWANIWA UNITED
KLABU ya Manchester United imeonesha nia ya kumnunua mchezaji wa Sporting Lisbon, Viktor Gyokeres, lakini wanahofia kwamba Liverpool inaweza kuharibu nafasi yao ya kumsajili mshambuliaji huyo wa Sweden mwenye umri wa miaka 25. (***HITC***)

### INACIO AWINDWA LIVER
LIVERPOOL inaweza kumsajili beki wa kati wa Sporting Lisbon na Ureno, Goncalo Inacio mwenye umri wa miaka 22, kwa pauni milioni 40. (***Football Insider***)

### PATTERSON ATAKIWA
LIVERPOOL imemtambua mlinda mlango wa Sunderland na England, Anthony Patterson mwenye miaka 23 kama mbadala wa mlinda lango wao wa Jamhuri ya Ireland, Caoimhin Kelleher, 25. ***(Mail)***


### SESKO KUNG'OLEWA LEIPZIG
KLABU ya Newcastle United inaendelea kumsaka mshambulizi wa RB Leipzig, Benjamin Sesko, huku ikipania kuishinda Manchester United na Chelsea katika kumsajili mshambuliaji huyo wa Slovenia, 20. ***(TeamTalks)***

### IOANNIDIS NA WEST HAM
WEST Ham imefanya uchunguzi kuhusu mshambuliaji wa Panathinaikos na Ugiriki, Fotis Ioannidis, 24. (***Football Insider***)

### MIRANDA NAYE ASAKWA
WEST Ham pia inamsaka Juan Miranda wa Real Betis, ingawa Brentford, Crystal Palace na Wolves pia zinamtaka beki huyo wa kushoto wa Hispania mwenye umri wa miaka 24. ***(HITC)***

### MUDRYK KUFUNGWA CHELSEA
CHELSEA imeanzisha harakati za kuongeza mkataba kwa kiungo wa kati wa Argentina, Enzo Fernandez na winga wa Ukraine, Mykhailo Mudryk, huku wachezaji wote wawili wenye umri wa miaka 23 wakiongezewa mwaka mwingine kwa mikataba ambayo tayari ilikuwa ya muda mrefu. ***(Sun)***

### AMRABAT AWANIWA
KLABU ya AC Milan imejulishwa kuhusu hali ya kiungo wa Fiorentina na Morocco, Sofyan Amrabat mwenye umri wa miaka 27, ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo Manchester United. ***(Rudy Galetti)***



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# BAYERN YAMTAKA ZIDANE

**MADRID,** Hispania

**●●● Tayari mawasiliano yamefanywa na kocha huyo ambaye amekuwa hana...**

KLABU ya Bayern Munich imewasiliana na Zinedine Zidane ili kumpa nafasi ya kuinoa timu hiyo msimu ujao, kwa mujibu wa ripoti nchini Hispania.

**Thomas Tuchel ataachana na timu hiyo msimu huu wa majira ya joto baada ya kusimamia kudorora kwa kiwango ambacho kimesababisha Bayer Leverkusen kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, huku maofisa wa Bayern wakitafuta mbadala wake.**

Kocha wa Leverkusen, Xabi Alonso, ndiye aliyekuwa analengwa zaidi kabla hajathibitisha hadharani nia yake ya kubaki na timu yake ya sasa, na kuwalazimu Bayern kutafuta kwingine.

Kwa mujibu wa gazeti la Marca, mawasiliano yamefanywa na Zidane, ambaye amekuwa hana kazi tangu alipoondoka Real Madrid mwaka 2021.


Mfaransa huyo anajulikana kuwa na nia ya kurejea kazini na ilisemekana kuwa anasubiri Timu ya Taifa ya Ufaransa, lakini Didier Deschamps ameongeza mkataba wake na 'Les Bleus' hao hadi 2026.

Hata hivyo, Zidane aliwahi kukiri kwamba hataki kufanya kazi katika nchi ambayo hawezi kuzungumza lugha yake kwa ufasaha na hivyo kuna uwezekano asihamie Ujerumani.

Jose Mourinho anatajwa kuwa mgombea anayetarajiwa kuinoa Bayern, pamoja na Julian Nagelsmann na Hansi Flick, ambao tayari wamefurahia vipindi vyao kule Bavaria.

Gazeti la Bild hivi karibuni iliripoti kwamba Nagelsmann, ambaye alifutwa kazi na na nafasi yake kuchukuliwa na Tuchel mnamo Machi 2023, sasa ndiye anayelengwa zaidi kwa kazi hiyo.

Kwa sasa Nagelsmann anainoa Timu ya Taifa ya Ujerumani, lakini mkataba wake utatamatika baada ya michuano ya Euro baadaye mwaka huu.




# RICE HAJAKATA TAMAA YA UBINGWA ARSENAL

**LONDON,** England

DECLAN Rice anaamini kuwa Arsenal bado ina nafasi ya kushinda Ligi Kuu England licha ya kufungwa na Aston Villa kwenye Uwanja wa Emirates Jumapili.

'Washikabunduki' hao walipewa nafasi ya kupanda kileleni mwa jedwali la ligi baada ya Liverpool kufungwa na Crystal Palace mapema siku hiyo.

Hata hivyo, ilikuwa Manchester City ambayo ilikuwa na kicheko cha mwisho baada ya wapinzani wote wawili wa taji kuanguka kwa kufungwa.

Villa walichukua pointi zote tatu kutoka kwa kikosi cha Mikel Arteta, mabao mawili ya dakika za lala salama kutoka kwa Leon Bailey na Ollie Watkins yakiiacha Arsenal pointi mbili nyuma ya City zikiwa zimesalia mechi sita.

Licha ya masikitiko hayo, kiungo wa kati Rice anafikiri Arsenal inapaswa kuwa na matumaini makubwa wanapojizatiti kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu.

Alisema: „Bado haijaisha, tupo katika nafasi isiyoaminika. Bado tuko tayari, bado tunazingatia kile tunachotaka kufanya na kile tunachoweza kufikia.

„Kutakuwa na misukosuko mingi zaidi kwenye Ligi Kuu. Lolote linaweza kutokea.

„Lazima tuendelee kuwa na mtazamo chanya. Tuna mechi sita za soka ambazo tunahitaji kutoa kila kitu kwa ajili yake na mambo mazuri bado yanaweza kutokea. Tunahitaji kujikita zaidi."

# Man City kamili kuivaa Madrid leo

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amekiri kuwa timu yake inapenda kucheza kwa shinikizo huku ikitarajia kuishinda Real Madrid katika mchezo wa mkondo wa pili wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, leo Jumatano.

City walishinda taji lao la kwanza la Ligi ya Mabingwa msimu uliopita kutokana na bao la Rodri kwenye fainali dhidi ya Inter, na kukamilisha mataji matatu ya kihistoria, wakiwa wamebeba Ligi Kuu England na FA.

Mhispania huyo anajinadi kuwa anataka kuwa kocha wa kwanza kuiongoza timu hiyo ya England kutwaa mataji mara tatu mfululizo, na wana nafasi kubwa ya kufanya hivyo baada ya matokeo ya wikiendi iliyopita kwenye Ligi Kuu.

Kwanza, City watahitaji kuwashinda mabingwa mara 14 Real Madrid kwenye Uwanja wa Etihad katika mchezo wa mkondo wa pili wa robo fainali baada ya kutoka sare ya mabao 3-3 kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu, na hakuna shaka akilini mwa Guardiola kwamba, wachezaji wake wana uwezo wa kukabiliana na matarajio.


„Walitushangaza katika mechi ya kwanza na nafasi za wachezaji na inabidi tuangalie," alisema Guardiola.

„Carlo Ancelotti pamoja na uzoefu wake, anaweza kufanya kitu tofauti na tunapaswa kuwa tayari. Lakini wakati huo huo, jaribu kuweka shinikizo kwako.

„Wachezaji wa City wanapenda shinikizo," aliongeza Guardiola husu mawazo ya wachezaji wake.

Kuhusu kama hiyo inamaanisha City, ambao sasa wanaongoza msimamo wa Ligi Kuu England baada ya kufungwa kwa Arsenal na Liverpool, watakuwa mabingwa wa nyumbani tena, aliongeza: „Hapana, hapana. Sisemi hivyo. Lakini tutashindana, hilo ni la uhakika."





# Pochettino akerwa na utoto wa wachezaji

**LONDON,** England

USHINDI wa mabao 6-0 ikiwa ni pamoja na usiku wa mabao manne kwa mmoja wachezaji wake nyota, Cole Palmer -ungemwacha Kocha wa Chelsea, Mauricio Pochettino, kuwa na furaha kubwa, lakini ilikuwa ni kinyume chake.

Kwani kocha huyo raia wa Argentina alikasirishwa na 'utoto' uliofanywa na wachezaji wake wa kugombea kupiga penalti kipindi cha pili huku Chelsea wakiwa tayari wanaongoza kwa mabao 4-0 dhidi ya Everton Jumatatu usiku kwenye Uwanja wa Stamford Bridge.

Nahodha Conor Gallagher alilazimika kuingilia kati kuwasukumia mbali Nicolas Jackson na Noni Madueke walipokuwa wakigombania mpira baada ya mchezaji huyo kuangushwa kwenye eneo la hatari.

Gallagher aliuchukua mpira huo kisha akampa Palmer, mpiga penalti aliyeteuliwa na timu.

„Wachezaji na wafanyakazi wanajua kuwa Cole Palmer ndiye mpigaji wetu wa penalti," alisema Pochettino aliyekasirishwa na kitendo hicho baada ya mechi.

„Nimesikitishwa sana na hali hiyo. Nidhamu ni kitu muhimu zaidi katika timu yetu.

„Sote tunakubali Jackson na Madueke walikosea. Sio wachezaji wazoefu. Ni vijana. Ilikuwa nzuri kwa Conor Gallagher kuamua.

„Hatuwezi kuonesha aina hiyo ya tabia," aliendelea. „Ni kama tuko shule, na kazi yetu ni kuwaonesha walichokosea ili wajifunze. Hakutakuwa na adhabu, lakini hii haiwezi kutokea tena. Palmer akiwa uwanjani ndiye mpigaji wa penalti."

Pochettino aliendelea kuomba radhi kwa tukio hilo na „picha mbaya" ya klabu ambayo iliwasilisha.

HABARI MICHEZO

# Azam, Mashujaa vita kali vya malengo leo

**Na Saada Akida**

AZAM FC leo inashuka dimbani kukabiliana na wegeni wao, Mashujaa FC katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi Dar es Salaam huku kila moja ikipigania malengo yake, moja ikitaka kumaliza nafasi ya pili na nyingine kujinusuru kushuka daraja.

Timu hizo zinakutana kwa mara ya pili, baada ya mwaka jana kukutana kwenye mzunguko wa kwanza ambapo Mashujaa FC wakiwa nyumbani walikubali kichapo cha mabao 3-0 katika Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Azam FC itashuka dimbani ikitoka kupata ushindi ugenini dhidi ya Namungo FC, kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi wakati Mashujaa FC wenyewe wakitoka kupoteza mechi nyumbani dhidi ya Coastal Union.

Kuelekea mchezo huo Kocha Mkuu wa Azam FC, Bruno Ferry, amesema wamejiandaa vizuri kwa mchezo wao wa leo dhidi ya Mashujaa baada ya kutoka kufanya vizuri dhidi ya Namungo FC.

Alisema mchezo huo ni muhimu kwao kutafuta pointi tatu kwa sababu wako kwenye vita vya kuwania nafasi ya pili na Simba, hivyo wakipoteza mechi hiyo watakuwa katika kipindi kigumu.

"Hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu wapinzani hawako nafasi nzuri na wametoka kupoteza, tutacheza kwa tahadhari kubwa na umakini ili kutafuta alama tatu dhidi ya Mashujaa FC, " alisema Ferry.

Kocha Mkuu wa Mashujaa FC, Mohammed Abdallah 'Bares', alisema wanakabiliwa na mechi ngumu na wanaingia kwa tahadhari kubwa ya kutafuta matokeo chanya dhidi ya Azam FC.

Alisema mchezo wa leo maana yake kubwa ni kutafuta matoke kwa sababu hali ya Mashujaa FC haiko katika nafasi nzuri na kulazimika kutafuta matokeo chanya.

"Hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu ukiangalia timu zote kila moja imekuwa na malengo yake kwa upande wetu kujiondoa katika nafasi ya chini, ambayo tupo kwa sasa," alisema Bares.

# WAWEKEZAJI NCHINI WATAKIWA KUCHANGAMKIA AFCON 2027

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, imewataka wawekezaji wa hapa nchini kuchangamkia fursa mbalimbali zitakazopatikana kutokana na Tanzania kuwa mwenyeji wa fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika zitakazofanyika mwaka 2027 (AFCON 2027).

Tanzania, Kenya na Uganda watakuwa wenyeji wa fainali za AFCON 2027.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, katika ufunguzi wa Kongamano la Uwekezaji kati ya Wadau wa Sekta ya Michezo na Utalii kuelekea AFCON 2027, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, alisema katika michezo kuna fursa kubwa na huu ni wakati wa wawekezaji wa ndani kujitokeza.

Msigwa alisema katika kuhakikisha huduma mbalimbali zinapatikana kwa kiwango bora, serikali imetenga viwanja 14 kwa ajili ya ujenzi wa hoteli eneo jirani na utakapojengwa uwanja wa kisasa jijini Arusha.

Alisema pia serikali tayari imeshaanza mchakato wa ujenzi mwingine wa uwanja wa kisasa katika Jiji la Dodoma huku tayati maboresho yakiwa yameshafanyika kwenye Uwanja wa Amaan uliko visiwani Zanzibar na umeshakaguliwa.

Katibu huyo alisema ili kuongeza fursa zaidi kupitia michezo, Tanzania inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mashindano ya dunia ya baiskeli ambayo yatafanyika jijini Arusha.

"Kutakuwa na fursa mbalimbali kabla ya AFCON, wakati wa AFCON na baada ya AFCON, wawekezaji wasiogope kuwekeza katika michezo," alisema Msigwa.

Aliongeza kwa kukipongeza Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kwa kuandaa kongamano hilo ambalo litasaidia kuongeza idadi ya wawekezaji wa ndani.

Naye Mkurugenzi wa TIC, Gilead Teri, alisema kituo chake kitasaidia wawekezaji mchakato wa kusajili kampuni, kujisajili na mfumo wa ulipaji kodi, kupata kitambulisho cha taifa na usaidizi wa eneo atakalochagua kama linaendana na uteuzi wake.

Alisema serikali imeweka maofisa wa pamoja ambao watamsaidia mwekezaji kupata leseni na kibali kwa ajili ya kuendesha shughuli anazotaka kufanya na kwamba TIC inapenda kuona asilimia 99 ya wawekezaji wakiwa ni Watanzania.

KAMBINI...




Wachezaji wa Simba wakiwasili Zanzibar jana kwa ajili ya kuweka kambi ya kujiandaa na mechi ya 'Dabi' ya Kariakoo, dhidi ya Yanga itakayopigwa Jumamosi wiki hii katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Mzize atamani kuifunga Simba

INATOKA UK. 24

ili kuzidi kuwafurahisha wanachama na mashabiki wa Yanga," alisema Mzize.

Katika mechi dhidi ya Singida Fountain Gate, Mzize alitoa pasi za mwisho zilizozaa mabao mawili, la pili na la tatu kwenye mchezo huo kwa Stephane Aziz Ki dakika ya 65 na Joseph Guede, dakika ya 67.

Katika mechi ya watani iliyopita ambayo ilichezwa Novemba 5, mwaka jana, alitoa ,asisti' mbili, moja kwa Aziz Ki, aliyefunga bao dakika ya 73 na nyingine kwa Maxi Nzengeli, akipachika bao dakika ya 77, na kuisaidia timu yake ya Yanga kupata ushindi wa mabao 5-1, mechi ikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Wakati Mzize akisema hayo, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi amesema anakitayarisha kikosi chake kwa ajili ya kupambana na timu ngumu ya Simba katika mechi ya watani wa jadi na si vinginevyo.

Alisema hawezi kusema kwamba wanaweza kushinda idadi ya mabao kama waliyoshinda mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Huwezi kusema utashinda mabao mengi au kama yale kwa sababu hata siku ile hakuna aliyetarajia kushinda idadi ile ya mabao, huu ni mpira na hii ni dabi, mimi nimeandaa kikosi changu kwa ajili ya kucheza mechi hiyo ili kushinda na kuwafurahisha mashabiki wetu, mengine huwa yanatokea hapo hapo uwanjani," alisema kocha huyo.

Yanga inakwenda kucheza mechi hiyo ikiwa imetoka kuibugiza Singida Fountain Gate mabao 3-0, huku watani zao wa jadi wakiwa na vikao vingi vinavyotokana na kutofanya vema kwenye michuano mbalimbali, Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la FA na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mabingwa hao watetezi, wanaongoza ligi wakiwa na pointi 55, ikicheza mechi 21, kushinda 18, sare moja na kupoteza mbili, ikiwa imeshapachika mabao 52 mpaka sasa.

Michezo
Jumatano Aprili 17, 2024
Nipashe



Bayern yamtaka Zidane UK. 21




## Mzize atamani kuifunga Simba

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Yanga, Clement Mzize amesema kiu yake ni kufunga bao katika mechi ya Jumamosi dhidi ya Simba.

Mzize ambaye katika mechi ya Jumapili iliyopita alitoa pasi mbili za mabao, Yanga ikishinda mabao 3-0 dhidi ya Singida Fountain Gate, Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, alisema baada ya kutoa 'asisti' mbili katika mechi hiyo, sasa anatamani kutupia katika mechi ya 'dabi', itakayochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi.

Straika huyo anaamini kuwa mchezaji anapofunga katika mechi ya 'dabi' basi rekodi inaendelea kubaki na kukumbukwa kwenye historia ya soka la Tanzania, pamoja na rekodi za michezo hiyo ya watani.

"Nimetumwa na wachezaji wenzangu, wameniambia niwaambie mashabiki wajae kwa wingi uwanjani ili tuwafurahishe, tusipowaona wao mioyo yetu inafifia, lakini tukiona wamejaa na wanatushangilia na sisi tunakuwa na morali ya hali ya juu sana.

"Naamini katika mechi ya Jumamosi tutapata ushindi, nakumbuka katika mechi dhidi ya Simba iliyopita 'niliasisti' mara mbili kama hii ya Singida Fountain Gate, sasa kwenye mechi hii naweza kufunga kabisa, natamani iwe hivyo

INAENDELEA UK. 23

# BENCHIKHA AWACHAMBUA WASHAMBULIAJI LIGI KUU

### ●●● Asikitika huku akiiongoza Simba kambini Zanzibar, asema tatizo hilo si...

**Na Saada Akida**

HUKU akikirejesha kikosi chake kambini visiwani Zanzibar kujiandaa na mechi ya 'Derby' ya Kariakoo dhidi ya Yanga, Kocha Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, amesema amegundua tatizo la kumalizia (ushambuliaji) ni janga la nchini kulingana na alivyoona timu nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Simba imerejea Zanzibar kuweka kambi kwa mechi hiyo ya Jumamosi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam saa 11:00 jioni, hiyo ikiwa ni mara ya pili msimu huu baada ya awali kujichimbia visiwani humo wakati wakijiandaa na mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Al Ahly ya Misri.

**Akizungumza na Nipashe jana, Benchikha alisema kazi kubwa ni kuhakiki sha anaendelea kuwapa mbinu wachezaji wake kuelekea mechi zilizosalia ikiwamo hiyo ya Kariakoo Derby dhidi ya Yanga.**

Benchikha alisema shida kubwa ya timu yake ni eneo la umaliziaji na kwamba hilo halipo kwenye timu yake pekee bali ni sehemu kubwa ya timu za Ligi ya Tanzania, lakini anahitaji kuendelea kujipanga kuhakikisha washambuliaji wake wanakuwa makini kwenye nafasi wanazotengeneza.

Alisema anaimani kubwa kutakuwa na mabadiliko katika eneo hilo kutokana na mbinu anazowapa katika mazoezi ikiwamo suala la kuwa makini kutumia nafasi hizo na kuweza kufunga.

"Hii tatizo si kwetu bali ni asilimia kubwa ya timu za ligi, lakini naangalia zaidi timu yangu, kuna nafasi nyingi tunazotengeneza tunashindwa kufunga, tunakuwa makini na hili kwa sasa ni kukaa na wachezaji kuwaeleza kuwa watulivu katika eneo hilo," alisema Benchikha.

Aliongeza kuwa anaimani baada ya msimu huu kufikia tamati, atafanyia kazi jambo hilo kwa kuhakikisha wanafanikiwa kuimarisha safu ya ushambuliaji na kuweza kutumia nafasi zinazopatikana.

Kocha huyo alisema mechi zijazo watafanya vizuri kwa kutafuta ushindi kwa kila mchezo ikiwamo dhidi ya Yanga ili kuendelea kujiweka pazuri kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara.

Wakati Benchikha akieleza hayo, imeelezwa kuwa kikao cha uongozi wa juu wa klabu hiyo kilichofanyika wiki iliyopita kikiongozwa na Mwekezaji na rais wa Heshima wa klabu hiyo, Mohamed 'Mo' Dewji, kimetoa mtihani kwa viongozi waliopo madarakani, kuhakikisha timu inapata matokeo mazuri katika mechi zijazo hususan Jumamosi dhidi ya Yanga.

"Ni kweli kikao kilikuwa kina mambo mengi, huku baadhi ya viongozi wakipewa mtihani kuhakikisha tunashinda mechi zilizosalia tukianza na Yanga na ili kufikia malengo ikiwamo kutwaa ubingwa au kushika nafasi ya pili," alisema mtoa habari huyo.

Kuhusu maboresho ya kikosi, alisema Benchikha amehakikishiwa kufanyiwa kazi mapendekezo yake ya msimu ujao ikiwamo suala la usajili kwa kuleta wachezaji wenye uwezo mkubwa hasa safu ya ushambuliaji.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >